# Uweza Mkamilifu Kwa Udhaifu Mkamilifu

Habari za asubuhi, marafiki. Ni vema kuwa nje tena asubuhi ya leo kwenye asubuhi hii yenye mvua, theluji, iliyochanganyikana. Nikijua kwamba wengi wenu mmekuwa na wakati mgumu wa kuendesha magari, mkitoka mbali. Nasi tuna baadhi ya ninii . . . hawa marafiki wa thamani wanaotoka Chicago na Alabama na Georgia na Tennessee na Illinois na kote huku, kwenye siku hizi, kwa hiyo tunaninii . . . tunatumaini ya kwamba Mungu atawapa ulinzi Wake mnaposafiri. Na ni maombi yetu kwamba atawalinda barabarani, kwenye barabara hizi hatari jinsi zinavyokuwa telezi katika wakati wa baridi kali. Na nchi hii ni mbaya wakati wa baridi kali. Ndiyo nchi ya kupendeza sana iliyopo wakati wa kuchipusha majani ama wa kupukutisha, bali wakati wa baridi kali na wakati wa kiangazi ni mbaya sana.

2 Sasa, sidhani wanarekodi bado mle ndani. Nami nataka tu kutoa tamshi kuhusu Jumapili iliyopita, katika ujumbe. Sababu ya mimi ku—kuizuia kanda wala nisingewaruhusu kuiuza hiyo kanda, kuitoa nje, vema, ni kwa sababu sina budi kuiangalia tena kwanza. Kwa sababu mara nyingi, kwa njia hiyo, ningesema mambo kwenye kanisa hili hapa ambayo nisingeyaweka mbele ya umma nje namna hiyo, kwa sababu wakati mwingine husababisha mawe ya kujikwaa. Na wakati mwingine hata husababisha maswali miongoni mwa watu wetu hapa maskanini. Na hiyo ni . . .

3 Sisemi hili . . . kusema mambo hayo kusudi niwe tofauti, lakini wakati mwingine chini ya upako unajua mambo ambayo usingeninii . . . usingethubutu kuwaambia watu. Halafu wakati mwingine chini ya upako jambo fulani litatokea, mnaona, wala hutajua. Na moja ya mambo ninayoamini yalisemwa (hiyo Jumapili iliyopita) ambalo linaweza kumfanya mtu . . . wakati nilipotaja ya kwamba kamwe sikuamini katika miito ya madhabahuni. Mnaona?

4 Ninataka kusema hilo na kulifafanua hilo mpate kuelewa. Kamwe hakukuwako na wito wa madhabahuni uliopata kufanywa katika Biblia nzima. Hakuna kitu kama hicho katika Maandiko. Hamna mahali kote katika nyakati ulipotolewa mpaka kwenye wakati wa Methodisti, yapata miaka mia mbili iliyopita, mnaona?

5 Miito ya madhabahuni ni wakati watu wanapokuja huku na kujaribu kuwashawishi na kuwavuta watu, "Njoo huku,

Yohana. Unajua, wao . . . Mama yako alikufa, akikuombea. Njoo huku, Yohana." Hiyo si imani, marafiki. La. Wa—wa aina hiyo, ninaninii . . . ni kwa nadra sana unasikia mmoja anayeenda mbali sana. Na, katika jambo hilo, unapata kila kitu. Hiyo ndiyo sababu kanisa limechanganyikiwa kabisa jinsi lilivyo leo hii, ni kwa sababu ya mambo kama hayo.

6 Imani, haikubidi kusema jambo moja, ndugu, Mungu yupo na tayari ametenda kazi. "Petro alipokuwa akisema Maneno haya Roho Mtakatifu akawashukia wale waliolisikia lile Neno." Unaona? Unaona? Unaona? Hakuna wito wa madhabahni, unaona, hakuna kitu kama hicho.

7 Sasa, madhabahu ndipo mahali pa kwanza pa maombi ambapo kila mtu anayekuja kanisani anapopaswa kuingia kwanza, apige magoti madhabahuni, aombe kimya kwa Mungu na kuomba dua ya maombi na—na kwa ajili ya wapendwa wao, na kumshukuru Mungu kwa ajili ya yale wamefanyiwa, kisha warudi kitini mwao.

8 Halafu kanisa ni mahali ambapo Neno la Mungu . . . "Nayo hukumu huanzia kwenye Nyumba ya Mungu," ambamo hukumu ya Neno hutolewa. Halafu . . . Lakini siku hizi, sisi—sisi tumebadilisha jambo hilo sana.

9 Sasa, sina neno dhidi ya mtu yeyote anayetoa miito ya madhabahuni, unaona. Hiyo ni . . . Nami mwenyewe nimetoa mingi, na huenda nitafanya mingi zaidi kama nikizidi kusonga mbele. Lakini kwa nafsi yangu tu . . . Unaona, u—u—unakusanya mengi mno. Wala hakuna neno dhidi yake, hamna udhuru ndani yake. Ni sawa. Unaona?

10 Maana, sikilizeni, Yesu alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu kwanza. Na wote alionipa Baba watakuja Kwangu." Hiyo ni kweli. Kwa hiyo basi, mnaona, wao ni . . . Hilo linatupilia wito wenu wa madhabahuni mbali kabisa. Mnaona? Mnaona hilo? "*Wote* ambao Baba . . . " Unaninii . . .

11 Jukumu le—letu ni "hubiri Neno." Biblia ilisema, "Wote walioamini walibatizwa." "Tubuni, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo, msamaha wa dhambi." Ati nini? "Mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi, mnaona, nanyi basi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."

12 Bali unapowashawishi na kuwavuta na kuwatisha watu, na kuwashawishi watu waingie . . . Watu hawana budi kuja kwa akili timamu, watulivu, kwa imani, na kumpokea Kristo. Ndipo jambo la kwanza wanalofanya mara wanapompokea Kristo wakiketi vitini mwao, jambo linalofuata ni kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la zile dhambi walizoshawishika kwamba wamefanya. Hivyo ndivyo wanavyoondolewa dhambi zao, mnaona. Kwa kuwa wametubu; wamebatizwa kama kumbukumbu kwa watu, kwamba, "Nimempokea Kristo kama

Mwokozi wangu binafsi"; basi wewe ni mtaradhia wa Roho Mtakatifu.

13 Na, sasa, watu wengi wanaendelea, kushawishi na kuwaita madhabahuni, na kadhalika namna hiyo, ambalo hilo ni sawa. Nitaambatana na jambo hilo, hilo ni sawa kabisa kwangu mimi, mtu yeyote anayetaka kufanya hilo. Lakini, kwangu mimi, si la Kimaandiko, mnaona, na kwa hiyo ni—ninapenda tu kudumu na Maandiko.

14 Na kwa hiyo sababu ya mimi kuishikilia kanda hiyo ilikuwa ni kwa sababu mkiitoa hiyo nje tungepokea barua mia tano kwa juma za kujibia. Kila. . .Hebu kanyaga tu desturi ndogo aliyo nayo mtu fulani, na hilo tu ndilo unalopaswa kufanya, ndipo yote yatasambaa tena.

15 Nami nafikiri, mara nyingi, kwamba mimi kidogo hupinga sana mambo mbalimbali kama hayo. Nami simaanishi kuwa hivyo, bali wakati mwingine wajibu unakuvuta hivyo, mnaona, u—unakufanya uegemee huko. Na kwa hiyo nina hakika watu wanafahamu jambo hilo.

16 Sasa, tunashukuru sana kwamba tungali tuna Baba mwema wa Mbinguni Ambaye—Ambaye huyapitia makosa yetu wala hatuhesabii sisi.

17 Nilikuwa nikisoma kwenye Kitabu cha—cha Warumi, mlango wa 4, ambapo Paulo aliandika wa—wasifu wa Kiungu wa maisha ya Ibrahimu. Sasa, tunajua ya kwamba Ibrahimu mara nyingi alivurugika kama tunavyofanya. Lakini wakati ninii. . . wasifu wake ulipoandikwa, hakukuwako na yoyote ya vurugu zake iliyotajwa, mnaona, hakuzitaja kamwe. Kasema:

> Ibrahimu *hakusitasita kwa kutokuamini ahadi ya Mungu; bali alitiwa nguvu. . .akimtukuza Mungu.*

18 Mnaona, na hivyo ndivyo ninavyotumaini wangu utaandikwa huko Juu, sio makosa yangu na kila kitu, bali yale tu ninayojaribu kufanya, kusudi la moyo wangu kuwafanyia watu wa Mungu.

19 Na sasa tumekuja asubuhi ya leo ku—kujaribu kuleta ujumbe mdogo hapa ambao labda Bwana ameuweka juu yetu kuutoa kwa watu. Na nikitumaini kwamba utawafaidi na kunifaidi mimi, maana tuko pamoja na tunaishi katika wakati wa ajabu sana, na siku za mwisho. Kwa hiyo kabla tu hatujaomba, ningetaka kusoma sehemu kadhaa katika Neno; moja kabla ya maombi, na moja baada ya maombi. Na kwanza, kuifungua ibada yetu kwa sehemu hii Yake, ningependa kusoma kutoka kwenye Kitabu cha Waebrania. Mlango wa 11 wa Waebrania, na ninii cha thelathi-. . .kifungu cha 32, kuanzia, kikizungumza kuhusu *imani.*

> *Nami niseme nini tena?* Ama *wakati usingenitosha kuleta habari za Gideoni,. . .na Baraka,. . .*

> *Samsoni,* . . . *Yeftha;* . . . *Daudi* . . . *Samweli, na za manabii;*
>
> *Ambao kwa imani walishinda milki za wafalme, walitenda haki, walipata* ahadi, *walifunga* kinywa *cha simba,*
>
> *Walizima nguvu za moto, waliokoka na makali ya upanga na walitiwa nguvu baada ya kuwa dhaifu, walikuwa hodari katika vita, walikimbiza* mgeni, *majeshi ya wageni.*
>
> *Wanawake walipokea wafu wao waliofufuliwa* . . . *wengine waliumizwa vibaya hata kuuawa, wasikubali ukombozi, ili wapate ufufuo ulio bora;*
>
> *Wengine walikuwa na* majaribio . . . *dhihaka* . . . kupigwa, *naam, kwa mafungo* . . . kufungwa gerezani*;*
>
> *Walipigwa kwa mawe,* wakakatwa *kwa misumeno,* wao *walijaribiwa, waliuawa kwa upanga; walizunguka-zunguka wakivaa ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi; walikuwa wahitaji,* . . . na *wakiteswa,*

20 Angalia haya yaliyotengwa:

> *(Watu ambao ulimwengu haukustahili kuwa nao:), walikuwa wakizunguka-zunguka katika nyika na katika milima na katika mapango na katika mashimo ya nchi.*
>
> . . . wote hawa *wakiisha kushuhudiwa kwa sababu ya imani yao, hawakuipokea ahadi;*
>
> *Kwa kuwa Mungu alikuwa ametangulia kutuwekea sisi kitu kilicho bora, ili wao wasikamilishwe pasipo sisi.*

21 Ninaposoma hadithi hizo za askari hao hodari, ninashangaa ni wapi ushuhuda wetu mdogo utakaposimama pamoja na watu hao kwenye Siku ile.

22 Kabla tu ya maombi, je! mtu yeyote angetaka kukumbukwa kwa Mungu? Inua tu mkono wako, na chochote unachohitaji naomba akione na kusikia na kukupa wewe sasa tunapoviinamisha vichwa vyetu.

23 Baba yetu mwenye neema na upendo, kwa unyenyekevu tunakikaribia Kiti Chako cha Enzi asubuhi ya leo katika Jina la Yesu, Mwanao, kuomba dua kwa ajili yetu na kwa ajili ya wengine. Wewe kwanza, Bwana, ungetusamehe makosa yetu yote na uovu wetu. Ndiposa tungewaombea wengine, Bwana, kwamba wao pia wasamehewe.

24 Nalo Kanisa Lako lingevutwa karibu zaidi Kwako. Kwani kwa kweli, Bwana, moyoni mwetu tunaamini ya kwamba Wewe uko tayari kutenda kazi pamoja na Kanisa Lako, ukiwa tayari kuliondoa ulimwenguni na kulihamisha kwenye Ufalme wa

Mungu. Lakini, Bwana, tusaidie tujifanye tayari kwa ajili ya wakati huo. Jalia asubuhi ya leo iwe ndio ule wakati, Bwana, kwamba kutoka mmoja kufikia sisi sote "Tutaweka kando kila mzigo mzito na dhambi ile ituzingayo kwa upesi, ili tupige mbio kwa subira katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu."

25 Nami ninaomba, Baba wa Mbinguni, leo, ya kwamba utawaponya wagonjwa na wanaoteseka. Wengi wanateseka kote nchini, na tauni, na "virusi" kama vile madaktari wanavyoviweka. Ninaomba ya kwamba nguvu Zako za uponyaji, Bwana, zitakuwa kwa hao watu.

26 Halafu kuja kwenye kusanyiko letu dogo hapa asubuhi ya leo. Wengi wameendesha magari mamia ya maili, wakianza jana usiku sana na usiku kucha na kuendelea asubuhi, leo hii, na kuendesha mbio wapate kufika maskanini. Na theluji inaanguka barabarani. Mungu, tunaomba ya kwamba utawabariki hasa wao. Hapana shaka iliwabidi wengi kutoa sehemu kubwa ya chakula chao cha juma lijalo, ama chochote kile, ama mambo ambayo wangeweza kutumia fedha zao kwayo, kwa petroli na kadhalika, wapate kuja.

27 Mungu, yeye akujiaye akiwa tupu ataondoka akiwa amejaa. Wewe uliahidi hilo. Nami ninaomba ya kwamba utaijaza mioyo yao na vikapu vyao (vya nafsi zao) vijae sana mambo mazuri ya Mungu hata wataondoka wakibubujika kwa "furaha isiyoneneka na iliyojaa Utukufu." Jalia tu vikombe vya watu hawa wa thamani vifurike, kwa mambo ya kiroho na mazuri kutoka kwa Mungu.

28 Bariki kila mkono, unajua mahitaji yaliyokuwa nyuma ya mkono huo, Bwana. Ninaomba kwamba utawabariki hasa. Tumekuona katika juma hili lililopita jinsi ambavyo ulijibu maombi kimiujiza katika dakika chache, wakati wa dharura na magonjwa na shida. Wewe ni Mungu, aliyepo kila mahali, anayewatetea watumishi Wake. Ninaomba, Mungu, ya kwamba utasimama na hawa asubuhi ya leo. Watimizie haja yao, Bwana, ya moyo wao. Siamini waliongozwa na jambo lolote la kichoyo, nia yo—yoyote mbaya. Ninaomba kwamba utawabariki.

29 Na sasa, Baba, nikumbuke mimi, sisi, leo, na jalia niweze kujiondoa njiani sana . . . Sisi sote, kuanzia mchungaji hata wa—watoto, jalia tuweze kujiweka kando juu ya madhabahu ya Mungu na kuifungua mioyo yetu na kumsikiliza Roho Mtakatifu jinsi atakavyonena na sisi. Geuza vyombo vyetu vya bara-. . . Zako kupokea baraka Zako, huku upande ulio bora ukiwa juu. Ndipo umimine nguvu za Mafuta ya kupaka ndani yao. Na utupe nguvu, Bwana, tunazohitaji kwa ajili ya siku zilizo mbele. Tujalie baraka hii. Tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

30 [Ndugu Branham anamjibu mtu fulani aliyemzungumzia juu ya simu iliyopigwa—Mh.] Hmm, sijui. Chukua tu namba yake ya simu umwambie nitampigia baada ya kanisa. Sijui.

31 Niombeeni. Ndugu Jack Moore kwenye simu, na angali akinishawishi niwe huko juma hili. Mnaona? Kamwe sisikii ninii. . .nikitaka kufanya hivyo, mnaona, na kwa hiyo sijui la kufanya. Ninampenda Ndugu Jack. Na ule mkutano mkubwa unaokuja huko chini naye aliwakatalia watu, kama vile Booth-Clibborn na wengineo, kuja. Kwa hiyo angali ameshikilia, aliweka matangazo yake na yote namna hiyo, akiningojea mimi nije. Kwa hiyo ni—ninapenda kujisikia nimesukumwa kweli kwenda, mnaona. Nami . . .

32 Na, sasa, tunapogeukia sasa tena kwenye Wakorintho wa Pili, nasi tutaanzia kwenye kifungu cha 12 cha Wakorintho wa Pili, na kusoma kifungu kimoja cha Maandiko kwa ajili ya somo, Bwana akipenda. Wakorintho wa Kwanza, ninii . . . Ama Wakorintho wa Pili, hasa, mlango wa 12 na kifungu cha 9. Ninataka kusoma fungu la kwanza . . . Ama fungu la pili la kifungu cha 9, sehemu yake.

> *Akaniambia, Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu . . .*

33 Hebu niisome tena sasa mpate kuwa na hakika kulipata somo hili:

> *Akaniambia,* (Huyu ni Mungu akinena na Paulo)*, Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu . . .*

34 Basi kama ningeliita somo, ningetaka kutumia hili, uweza . . . *Uweza Mkamilifu Kwa Udhaifu Mkamilifu.* Kama tuna udhaifu tuna uweza. Ni somo lisilo la kawaida kwenye . . . katika kusanyiko la Kipentekoste, kufanya . . . kuchukua somo la *udhaifu*, kwa kuwa daima tunashuhudia "tuna nguvu sana."

35 Nami nimesema hapo kabla, ya kwamba, mimi hujaribu tu kuomba juma zima nione ni lipi lingekuwa jema kwangu kulileta mbele ya kusanyiko. Kama ilikuwa ni kuja tu hapa nipate kusikiwa, ni afadhali nimsikie mtu mwingine yeyote asubuhi ya leo akisimama hapa.

36 Kwa kweli, mpaka kufikia siku chache zilizopita, nilikuwa huko chini Kentucky pamoja na watu wa Ndugu Gabehart kule. Nilipokuwa nimeondoka kwao, ndugu huyu wa thamani na mke wake na familia na hao wengine, mpaka nikalishika wazo hili.

37 Nilikuwa nimeingia kwenye nyumba fulani kidogo tu kabla ya hapo. Nilikuwa nimesimama nje, ndipo mama huyo akasema, "Ningetaka kuzungumza na mhudumu yule." Nami nikaingia kwenye maskini nyumba yao ndogo. Na kulikuwako . . . Yeye akasema, "Wewe ni Ndugu Branham?"

Nami nikasema, "Naam, mama."

38 Akasema, "Ninaona aibu jinsi nyumba yangu ilivyo," naye akasema, "kukuomba uingie." Akaanza kulia. Akasema, "Lakini ni—nina haja sana na nina imani sana kwako."

39 Nami nikakuta kwamba ilikuwa ni ambako maskini Dada yetu Cox ambaye tunakaa naye kidogo huko chi—chini, ma—maskini bikizee aliye na kinasa sauti akipitia kwa majirani akicheza kanda. Jambo ndilo hilo! Wazo ndilo hilo! Mnaona?

40 Niliangalia kila mahali katika nyumba hii, maskini nyumba ndogo duni, karibu kama ile niliyolelewa, bali ukuta umejaa picha za Kristo. Palikuwapo na Biblia mezani. Nikasema, "Kamwe sijapata heshima zaidi maishani mwangu, hii ndiyo aina ya nyumba ninayopenda kuingia." Akauliza maombi kwa mtu fulani. Na saa tano tangu wakati tulipoomba pamoja, mimi na maskini bikizee huyu tulipoomba pamoja, Mungu alikuwa amelijibu.

41 Kwa hiyo tukaomba tena, na mimi na Mama Cox na hao wengine mezani asubuhi hiyo, tulikuwa tumeinama na kumwomba Mungu atupe nafasi kufanya jambo fulani kupitia jitihada alizokuwa amefanya. Na, kwa kuombea jambo hilo, Mungu akafungua njia. Mnaona? Yeye ni Mungu!

42 Sisi hujaribu kufanya udhaifu wetu kuwa udhuru. Tunataka kusema jinsi tulivyo wakubwa, jinsi tulivyo wakuu. Nafikiri hilo ndilo moja la mambo ambayo mimi . . . Sababu ya Mungu kunipa somo hili, ilikuwa ni tutoe hilo akilini mwetu. Mnaona?

43 Yapo mambo madogo tunayofanya. Na hiyo ndiyo sababu tunakuja kanisani, ni kutaka kujua mahali makosa yetu yalipo, na mambo ambayo tunaweza kujiboresha kwayo. Kama tukija kanisani kwa lingine lolote—kusudi lingine lolote zaidi ya hili, ninahofia hatutapata mengi sana kutokana na kuja kanisani. Hatuna budi kuja kutafuta kujua udhaifu wetu, kutafuta kujua mahali petu pabaya na ninii yetu . . . jinsi . . . tuone jinsi tulivyo wadogo, na kuweka matumaini yetu juu ya Mtu aliye na nguvu. Ila tunapokuwa na udhaifu . . .

44 Wapo wengi wetu wanaopenda kushuhudia ama wanaopenda kuwazia ya kwamba hatujitoshelezi na, kwa hiyo, tunafanya huo kuwa udhuru, "Sina elimu, sina kipaji, siwezi kufanya jambo *hili*." Na kama ukiendelea na hilo na kufanya hilo kwa njia hiyo, uendelee namna hiyo, basi huwezi ukawa kitu chochote. Lakini jambo lile lile tunalolitolea udhuru, kwa udhaifu wetu, Mungu hutumia jambo lilo hilo kufanyia kazi. Mnaona? Yeye hutungojea tuifikie hali hiyo apate kututumia. Tu—tunachukua udhuru na kusema, "Vema, mimi—mimi—mimi—mimi—mimi . . . siwezi kufanya jambo hili, sijiwezi. Si—siwezi kulifanya." Naye Mungu anachukua jambo lilo hilo kufanya kazi nalo. Hiyo ni kweli.

45 Hiyo ndiyo sababu Yeye—Yeye hutuchagua, kwa kuwa tuko katika hali hiyo. Sasa, hilo linasikika la ajabu, bali dakika chache tu tutafikia kwenye sababu yake, Mungu akipenda.

46 Tu—tunaona, kama tu ambavyo tumekuwa tukisoma, ya kwamba udhaifu na kukataliwa . . . na tunaona ya kwamba hao

watu walio dhaifu sana na kukataliwa na ulimwengu wa nje, ndio mashujaa wa Mungu, wanaopata ushindi kwenye mstari wa mbele, anawachukua wale walio—walio . . . wanaojisikia hawastahili.

47 Palikuwapo na ndugu wa Kimethodisti, watatu wao wanaohudhuria kanisa hili kutoka huko Ohio, ama kaskazini mwa Indiana. Waliniambia sio muda mrefu uliopita, kasema, "Ndugu Branham," kasema, "ndio kwanza tumpokee Roho Mtakatifu, je! sasa tutafute karama kwa ajili ya huduma yetu?"

Nikasema, "Msifanye hivyo! Achaneni nazo."

48 Ndipo akageuka na kuniangalia, kasema, "Ndio kwanza nisome kitabu cha ndugu fulani kilichotwambia baada ya kumpokea Roho Mtakatifu inatupasa 'kuzitafuta karama,' kwa ajili ya hizi kumtumia huyu Roho Mtakatifu."

Nikasema, "Ndipo mwe na kiburi!" Mnaona?

49 Kama ukiangalia katika Biblia, daima ni wale wanaojaribu kuiepa, ndio Mungu huwatumia. Mradi tu mtu ananinii . . . anataka kufanya jambo fulani na anadhani ana kipaji cha kutosha anachoweza kutumia kwenye kazi hiyo, Mungu kamwe hawezi kumtumia mtu huyo. Mwangalie Musa, akitoroka; mwangalie Paulo, akitoroka; na hao wengine, wakijaribu kuiepa.

50 Nikasema, "Usitafute chochote. Mungu akiwa na chochote kwa ajili yako, Yeye atakupa." Unaona? "Na mwache tu—mwache ashughulikie hilo." Nikasema, "Ndipo unafikia baadhi ya nyakati hizi kama tulizo nazo, tulizo nazo leo, ambapo kila mtu anataka kufanya *hili* na kufanya *lile* na kuwa mtu mkuu. Angalieni yale tuliyoingia pamoja na hayo, mnaona."

51 Badala ya kujaribu kuwa wakuu inatupasa kujaribu—kujaribu kupata kujua jinsi tunavyoweza kuwa wadogo. Unaona? Ndipo Mungu anaweza kututumia. Nina Maandiko kadhaa yaliyoandikwa hapa ambayo inanipasa kuwa nikiyarejea, nadhani, bali ninaninii . . . sisi . . . Huenda nisipate wakati wa kufanya hivyo. Lakini tunaninii . . .

52 Angalia kwamba inachukua wa—walio wanyonge kuliko wote na waliokataliwa, na kwa kweli kila shujaa Mungu aliyepata kuwa naye kwenye mstari wa mbele wa vita alikuwa ni mtu wa jinsi hiyo. Mtu aliyekuwa amekataliwa, mtu aliyedhani hajitoshelezi, mtu asiyekuwa na kipaji hata kidogo, basi mtu huyo yuko katika hali nzuri kwa hiyo Mungu anaweza kuanza kumtumia. Hiyo ni kweli. Ni wakati wanapojisikia kana kwamba hawawezi, hawana kitu, hapo ndipo Mungu anapoweza kuwashika na kufanya kitu nao. Mnaona? Wakati . . . Lakini wakati tunapowazia ya kwamba tunaweza kulifanya, basi Mungu hawezi kututumia kwa kuwa tunataka kulifanya sisi wenyewe.

53 Na, basi, upande huo mwingine, tunapata hisi hizi nasi tunafikiri basi kwamba hatustahili, wala hatutaki kulifanya; lakini basi kama tukiusikiliza tu mwito wa Mungu, hilo ndilo jambo lenyewe ambalo Mungu anatutaka tuliingilie, hali ya namna hiyo, kusudi Yeye aweze.

54 Tunapokuwa hatustahili, sisi wenyewe, ndipo tunaweza kujitolea kwa Roho wa Mungu. Mradi tu tunafikiri ya kwamba tunaweza kulifanya, basi hatuwezi kulifanya. Bali tunapofikia mahali ambapo tunajua hatuwezi kulifanya, basi tunajitolea wenyewe kwa Mungu na Yeye analifanya. Kwa hiyo basi kama ni sisi tunaojaribu kulifanya tutashindwa, bali ikiwa tu tutajitolea kwa Mungu basi Mungu hawezi kushindwa. Kuna jambo moja pekee ambalo Mungu hawezi kufanya, na, hilo ni kushindwa. Yeye anaweza kufanya jambo lingine lolote ila kushindwa. Bali Yeye hawezi kushindwa.

55 Kwa hiyo mradi tu tunajaribu sisi wenyewe na kutegemea vipaji vyetu wenyewe, na kadhalika, vema, hatutafanya kitu. Lakini tunapofikia mahali ambapo tunafahamu sisi si kitu, basi Mungu anaweza kututumia.

56 Jambo muhimu, moja la mambo muhimu ambayo inatubidi kuyafahamu. . . Sasa kumbukeni hili, na zaidi sana ninyi wahubiri vijana, na watu wa kawaida pia. Kuna jambo moja linalotubidi kulifahamu kama tunatarajia kutimiza mapenzi ya Mungu maishani mwetu, hilo ni, inatubidi kufahamu wazo la *kipaji cha kibinadamu*. Kama kamwe tukifikia mahali ambapo tunawazia ya kwamba tunaweza kulifanya kwa akili zetu wenyewe na vipaji vyetu wenyewe, inatupasa kuelewa hilo hivi kwamba tunaweza kuondolea mbali jambo hilo na kuliweka kando kusudi Mungu aweze kututumia. Hiyo ni kweli.

57 Na kujitolea kabisa! Hatuwezi kutumia hata kipaji kimoja. Inatupasa kujitolea kabisa! Na, kumjia Mungu, inakubidi kusalimisha Kwake nafsi, mwili, na roho pia. Kila kitu ulicho wewe hakina budi kusalimishwa kwa Mungu, kusudi aweze kufanya mapenzi Yake ndani yako na ndani yangu.

58 Sasa, hilo ni gumu, ninajua, maana daima tunataka kuchangia sehemu yetu ndani yake, jambo fulani *tunalojua*, tunajua ya kwamba tunataka kulifanya. Tunasema, "Vema, na—najua tu linapaswa kufanywa hivi." Lakini mradi tu unalifanya jinsi hiyo litakuwa ni makosa, na Mungu kamwe hatatumia jitihada hiyo. Labda (msaada wa Bwana) tutalifikia hilo katika dakika chache, na kukuonyesha tu jinsi ambavyo Mungu hawezi kutumia kipaji chako.

59 Na hiyo ndiyo shida ya ulimwengu siku hizi: kuna ujuzi mwingi sana wa seminari, mwingi sana umewekwa juu ya elimu, mwingi sana umewekwa juu ya uhusiano ama ushirika katika dhehebu, tunategemeana sisi kwa sisi, tunawategemea watu wenye kipaji.

60 Biblia ilisema, "Mnawezaje kuwa na imani wakati mnaninii—wakati ninyi. . . " Hebu tuone, Andiko hilo likoje? "Mwawezaje kuwa na imani wakati mnapendeleana mmoja kwa mwingine?"

61 Wakati tunapotarajia, tukisema, "Jamaa huyu, yeye ni mtu mashuhuri. Huyu ni mtu mashuhuri, nitamwegemea tu," hilo halimpendezi Mungu wakati ukifanya hivyo. Hatuna budi kumwegemea Mungu na Mungu peke yake! Hatupaswi kutegemea kipaji chetu wala cha mtu yeyote. Lazima tujisalimishe kabisa kwa Mungu.

62 Hamna kipaji, sijali ni cha nani, kitakachopata kutumika mbele za Mungu. Mungu hana budi kuondoa vipaji vyetu vyote kutoka kwetu kabla hajafanikisha kusudi Lake. Kama ana jambo fulani la sisi kufanya, na mradi tu tunajisikia tunafanya kazi nzuri sana kwa hilo, basi kamwe hatutaweza kutumiwa na Mungu.

63 Sasa, unasema, "Unatoa tamshi la kijumla sana hapo, Ndugu Branham." Na hilo—hilo ni la kijumla, lakini hebu angalia kote huku uone kama ni kweli ama si kweli.

64 Angalia kote leo hii kwenye mafanikio yetu yote makuu tunayowazia tumefanya, na je! Ukristo uko wapi Marekani? Angalia makanisa yetu yote na madhehebu, na wainjilisti wetu na miamsho ya uponyaji, na kila kitu ambacho tumekuwa nacho, basi ni kitu gani? Ni mbaya kuliko ilivyopata kuwa hapo mwanzo! Ni mbaya leo kuliko ilivyowahi kuwa, kwa sababu tumejaribu kulifanya kwa kipaji cha kibinadamu.

65 Wanakusanyika pamoja na kufanya maombi marefu na kutoka hapa nje. Na ilikuwa ni hivi majuzi ambapo walikuwa na wengi sana, mia moja na hamsini elfu, ama kitu kama hicho, wamekusanyika pamoja, Protestanti na Katoliki pia; kukariri maombi kadhaa, na kuomba maombi kadhaa, na kufanya maombi fulani, na kadhalika. Hao ni afadhali hata wasingekusanyika, hayafai kitu machoni pa Mungu.

66 Sasa, kama nikiwa mkosoaji, samahani. Mnaona? Lakini ni—ninaninii. . .Inakubidi kusindilia jambo hilo. Unaona? Inakubidi kulifanya wazi kabisa.

67 Basi ilikuwa na faida gani? Hamna. Wala haitakuwa mpaka kila mtu anayekiri kuwa ni Mkristo atasahau kipaji chake mwenyewe na kujitolea kwa Mungu.

68 Ndipo Mungu anapoweza kutimiliza kusudi Lake kwa kutuma. . .sio ufufuo, bali, ndugu, kile anachopaswa kufanya kwanza ni kutuma mauaji, hiyo ni kweli, kusudi *tuweze* kufufuka. Huna budi kufa kabla hujazaliwa mara ya pili, nawe huna budi kuninii. . .Yeye anahitaji mauaji yetu. Maskani hii inahitaji mauaji, nami pamoja nayo. Sisi sote, tunahitaji ma—mauaji ili tuweze kufufuliwa katika maisha mapya, mshikilio

mpya, tumaini jipya, tukio jipya! Kwanza tunahitaji siku ya maombolezo.

69 Tunahitaji mahali pa kujitolea kwa Roho badala ya kutegemea sana elimu na ratiba zetu, nasi. . .miamsho yetu na yote tuliyo nayo. Tu—tu—tunategemea ushirikiano na wahudumu wengi sana mbalimbali kushirikiana. Tunaruhusu wengi sana. . . "Kama hatuwezi kupata idadi fulani, mbona, hatutaufanya. Hatutaenda kwenye miji bila hiyo." Halafu basi, tunapofanya hivyo, tunafanya mtambo mkubwa mno ulio na mnoko wa kaboni ndani yake, mnaona.

70 Kwa hiyo i—inatupasa kukiacha hicho, hicho kipaji cha kibinadamu. Inatupasa kufikia mahali ambapo tunaweza kuzisalimisha nafsi zetu na maisha yetu, hata kwa mke nyumbani, kwa mkulima, kwa makanika, ama yeyote tuliye, inatupasa kujisalimisha kabisa kwa Mungu na kujua ya kwamba "sisi si kitu." Ndipo tumwache Mungu aanzie hapo. Ndipo anaanza kusogea, kutenda kazi. Na hiyo inatujumuisha sisi sote, kila mmoja. Hilo ndilo ja—jambo tunalopaswa kufanya.

71 Historia inathibitisha, inathibitisha sasa, inathibitisha (historia inathibitisha) ya kwamba Mungu daima aliwachagua watu duni wapate kuwa watu Wake wa maana. Mungu humchukua mtu duni.

72 Leo hii, isipokuwa uwe na msingi mzuri wa kitheolojia, afadhali hata usijaribu kuukaribia mji, afadhali hata usijaribu kuukaribia mkutano. Lakini kama una misingi bora, pamoja na mafunzo makuu na kadhalika nyuma yako, unaweza kuingia katika mji wowote na kupata ushirikiano, ufanye mkutano mkubwa. Vema, si mkutano. . .Ni mkutano, kama kitu kingine chochote, bali una faida gani? Unaona, u—ungali. . . Unawapata hawa wasichana wadogo na wavulana wadogo wanaokuja, wakitafuna—wakitafuna chingamu na kupanda kwenda madhabahuni, na wanawake na wanaume wakipanda kwenda huko kusema tu "walipanda kwenda madhabahuni," wanaingia chumbani kushauriwa kisha wanarudi na kunyunyiziwa ama kuzamishwa, ama vyovyote walivyo, na ninii—na mwaka mmoja tangu hapo. . .

73 Mmoja wa wainjilisti wetu mashuhuri sana alisema, kama angeweza kujua ya kwamba angeweza kudumisha asilimia kumi ya waongofu wake kwa mwaka mmoja, angefurahi. Wakati, basi, wakati kama angalikuwa na waongofu elfu moja, mwaka ujao kunapaswa kuwa, ambapo pangekuwako na elfu kumi wa hao. Mnaona, tunakosa shabaha, tunakosa lengo.

74 Wengine wetu wanalijenga juu ya wazo la kiakili, "Loo" hiyo, "huyu mjua yote, mtu huyu ni msomi aliyefunzwa. Tunapaswa kuwafunza watu wetu na kuwaelimisha."

75 Huyo mwingine analiwekea msingi juu ya mhemko fulani wa—wa mwenendo, kutetemeka, kulia, kupaza sauti, kucheza

katika Roho, ama kitu fulani, kazi ya nje ya mhemko. Na hiyo ni mbaya tu kama elimu! Iwapo ibilisi hawezi kukupata upande *huu*, yeye atakusukumia upande *ule*.

76 Lakini jambo ni kwamba, ni kutokuwa na kitu unachoweza kutegemea ndani yako mwenyewe wala lolote unaloweza kufanya, kusalimisha tu kabisa udhaifu wako kwa Mungu, na kusema, "Mimi hapa." Usiwe na kitu, usiwe na kipaji unachoweza kutegemea!

77 Tafuta kote katika Maandiko uone, kama vile nilivyo na Maandiko yaliyoandikwa hapa ninayorejea. Huku nyuma katika Maandiko, tunaona, ya kwamba Mungu daima alitumia watu duni wapate kufanyika watu Wake wa maana. Yeye daima aliwachukua wale ambao ulimwengu ulikuwa umewakataa, waliokataliwa na wakati wa kisasa, na hao ndio Yeye aliowachukua akawatumie.

78 Watafakarini mi—mitume. Tafakarini juu ya Petro, mvua samaki, hana elimu ya kutosha kuandika jina lake mwenyewe. Yohana, asiye na elimu wala maarifa. Watu hao! Yeye aliwakwepa watu mashuhuri na makuhani walioelimika na watu maarufu wa siku hizo, wasomi, washiriki wa kanisa, na akapitia. . .hao watu waliodhania walikuwa watu mashuhuri, kisha akawachukua hao waliokuwa ni watu duni akawatumia.

79 Sasa, mtu mashuhuri anaweza kuwa mmoja wa watu Wake, Mungu anaweza akawatumia kama wako tayari kusahau kwamba wao ni watu mashuhuri. Kama uko tayari kusahau ya kwamba wewe ni mtu *mashuhuri* na uwe *duni*, basi Mungu anaweza kukutumia na kufanya mtu mashuhuri kutoka kwako. Unaona? Lakini huna budi kusahau ya kwamba wewe ni mtu wa maana sana.

80 Wapo wengi wetu, wengi wetu hufanya hivyo ma—maishani mwetu. Mara. . .Watu wengine, mara wanapokuwa ni Wakristo, wanaingiwa na kiburi, kutokujali, hiyo ni kweli, wakati wanachukua njia nyingine. Wanarudi nyuma badala ya kwenda mbele. Wakati. . .Kadiri unavyoweza kutoa katika nafsi yako, ndivyo unavyopata nafasi zaidi kwa ajili ya Roho Mtakatifu kuingia.

81 Kama vile Elisha alivyomwambia Yehoshafati na hao wengine, kasema, "Fanyeni bonde hili lijae mahandaki. Kadiri mtakavyochimba chini, ndivyo mtakavyopata nafasi kubwa ya maji." Na kadiri tunavyoweza kutupilia mbali nafsi zetu, u—upuuzi wa vipaji vyetu wenyewe, ndivyo patakavyokuwapo na nafasi zaidi ya kujazwa na Roho wa Mungu; almradi tunaweza kufanya jambo hilo.

82 Paulo, yule ndiyo kwanza tusome habari zake hapa katika—katika Wakorintho, katika Wakorintho wa Pili, tunaona ya kwamba mtu huyu alikuwa ni mtu mashuhuri. Alikuwa ni

msomi, mtu mashuhuri. Lakini ilibidi asahau yote aliyopata kujua, kusudi amjue Kristo.

83 Nitaninii. . .nitasoma moja ya Maandiko haya hapa, ili kwamba m—mnataka kusoma pamoja na mimi. Hebu tugeukie Wakorintho wa Kwanza, mlango wa pili na kifungu cha kwanza, kwa dakika moja. Na hebu tusome hapa kwa dakika moja tu yale Paulo aliyosema, mtu huyu msomi mkuu, yale aliyosema kuhusu nafsi yake, yale yaliyombidi kufanya. Wakorintho wa Kwanza, m—mlango wa pili wa Wakorintho wa Kwanza, na tuanzie kwenye kifungu cha kwanza. Msikilizeni huyu msomi.

84 Mtu huyu alikuwa amefunzwa. Angeweza kuzungumza karibu kila lugha iliyokuwapo ulimwenguni. Ilimbidi kujisifu juu yake. Alilelewa chini ya dhehebu kali la Mafarisayo, na baba yake alikuwa Farisayo. Baadaye alikuwa ni "Farisayo wa Mafarisayo," na hiyo inamaanisha ya kwamba alikuwa—alikuwa ndiye Farisayo aliyekuwa m—mkali sana. Alikuwa ni jamaa mashuhuri. Naye alikuwa na mamlaka, na alikuwa ni mwerevu.

85 Baba yake alikuwa amempa elimu chini ya mwalimu hodari kuliko wote aliyekuwako nchini, Gamalieli, wakati huo akiwa ndiye mwalimu maarufu kuliko wote wa shule zozote. Paulo akawa mtu wa namna hiyo. Alijifunza kila lugha. Alijifunza saikolojia. Alijifunza mambo yote mbalimbali yaliyokuwako katika—katika. . .yaliyopaswa kusomwa kwa njia hiyo. Naye aliegemea sana kwenye—kwenye maskani ya—ya makuhani na pamoja na mtu ma—mashuhuri. Naye alikuwa akienda huku na huku akilitesa sana Kanisa.

86 Msikilize mtu yuyu huyu, akiwa na elimu hii yote, akiisha kumpokea Kristo. Sikilizeni yale aliyosema. Jinsi alivyokuwa mwenye nguvu na mtu mashuhuri, ilimbidi kusahau hilo. Ilimbidi kutambua ya kwamba asingeweza kujitegemea mwenyewe. Ilimbidi kutambua ya kwamba elimu yake ilikuwa ni bure. Ilimbidi kutambua, ya kwamba mafunzo yote aliyopata kuwa nayo, ilimbidi kusahau kila kitu alichopata kufunzwa. Msikilizeni sasa.

> *. . .mimi, ndugu zangu, mimi* nilipokuja *kwenu,. . . sikuja niwahubiri siri ya Mungu kwa ufasaha wa maneno,. . .kwa hekima.*

"Kamwe sikuja kwenu kuwaambia, 'Sasa, mimi ni Daktari Sauli kutoka Shule ya *Ninii*, mimi ni. . .kutoka kwenye shirika kuu la dhehebu hili.' Kamwe sikuja kwenu jinsi hiyo."

> *Maana naliazimu nisijue neno lo lote kwenu ila Yesu Kristo, naye amesulibiwa.*

87 Hapo, sikilizeni ushuhuda wa mtu kama huyo.

"Nimeazimu nisijue neno juu ya vipaji vyenu. Ninajua hamna kitu ndani yenu nami nimeazimu tu kujua jambo moja ninaloliona ndani yenu, hilo ni Yesu Kristo Naye

amesulibiwa. Mwokozi aliyesulibiwa miongoni mwenu, huyo tu Ndiye nitakayemtambua.”

88 Msikilizeni.

> *Nami nilikuwako kwenu katika. . .(*ukuu? Katika nini?*). . .hali ya udhaifu na hofu na. . .matetemeko mengi.*

89 Mngeweza kuwazia mtu, Farisayo wa Mafarisayo, mwalimu wa waalimu, mtu aliyefunzwa kutoka utotoni (kwa ajili ya huduma) apate kuwa mtu mwenye ufasaha aliyekuwa mwenye akili na mwerevu sana, kuja mbele ya tabaka la watu kama Wakorintho na kusema, “Nilikuwa kwenu katika hali ya udhaifu, na katika hofu, na matetemeko mengi”? Mtu aliyeupindua ulimwengu juu chini, mmishenari mashuhuri sana aliyepata kujulikana, alikiri ya kwamba yeye “alikuja katika hali ya udhaifu,” sio kama msomi aliyefunzwa, bali “katika hali ya udhaifu, katika hofu,” asije akaondoka Njiani mahali fulani. “Katika matetemeko mengi,” kwa kuwa asingeweza kutegemea kipaji chake mwenyewe.

90 Sababu ya yeye kuwa na “hofu,” sio kwa sababu aliogopa chochote, bali alihofu angemuudhi Mungu kwa njia fulani, kwamba angekichanganya kipaji chake ndani Yake; kitu ambacho alikuwa amejifunza, ambacho alikuwa. . .Yeye alikuwa akiwaambia ya kwamba, “Sikuja kwenu kwa huu ufasaha wa maneno (nilikuja kwenu *nikihofu* kwamba ningekuja namna hiyo), bali nilikuja kwenu pasipo kujua kitu ila Kristo, Naye amesulibiwa.”

> *Nami* nilikuja kwenu *katika* hofu, na udhaifu*, na matetemeko mengi.*

> *Na ujumbe wangu na kuhubiri kwangu hakukuwa kwa maneno ya hekima ya mwanadamu yenye kushawishi akili za watu, bali kwa dalili za Roho na. . .nguvu:*

91 Msikilizeni mtu huyu aliyekuwa shujaa aliyejivua mwenyewe. Amina! Kama kuna jambo lolote shule zetu zinalohitaji leo hii, kama ni kitu makanisa yetu yanachohitaji leo hii, ni kujivua, mawazo yenu wenyewe na vipaji vyenu. Jivueni mbele za Mungu msije mkajaribu kufanya jambo fulani ndani yenu wenyewe.

92 Ninatumaini ninyi. . .hilo linaingia ndani yetu, hapa na kwenye ulimwengu wa kanda, pia, kwamba unatambua ya kwamba huna budi kuwa bure. Sio mjuaji, sio mtu fulani mashuhuri, bali *mtu duni*. Wewe kuwa. . .huna budi kuwa mavumbi. Huna budi kufikia mahali ambapo unajua ya kwamba wewe si kitu. Wala kamwe usiinuke juu yake, kwa maana mara unapoinuka juu yake unainuka juu ya Mungu. Inakubidi kujidumisha kwenye mavumbi na kwenye barabara ya kwenda Dameski. Inakubidi kujitoa kwenye majisifu yako. Na hiyo ni kwa kila mahali, hapa na kwenye ulimwengu wa kanda.

93 "Ujumbe wangu," yeye alisema, "hauninii. . .kwa maneno ya kushawishi ya mwanadamu na hekima ya mwanadamu, bali katika dhihirisho la nguvu za Roho."

94 Sasa angalieni! "Kwa ajili gani, Paulo? Kwa nini unafanya hivi?"

> Nguvu! *Ili imani yenu isiwe katika hekima ya wanadamu, bali katika nguvu za Mungu.*

95 Loo, ni mhubiri wa jinsi gani! Mtu huyu mashuhuri ambaye. . .Yeye alimtafuta Mungu, naye akasema, "Mungu, mimi ni dhaifu na si—sijui la kufanya. Ninakuomba tu, Mungu, kunitia nguvu na kuniondolea udhaifu wangu, na mambo haya, kusudi niweze kuwa na nguvu zaidi."

96 Mungu akamjibu, kasema, "Paulo, uweza Wangu hutimilika katika udhaifu wako."

97 Ndipo Paulo akasema, "Ninapokuwa dhaifu basi nina nguvu. Naam!" Akasema, "Basi nitaninii. . .nitajisifia udhaifu wa udhaifu wangu na kadhalika. Ninamshukuru Mungu kwamba niliyaondoa yote kwangu. Na ninapotoa kila kitu ndani yangu, ndipo Mungu anapoweza kuingia. Lakini mradi nina baadhi ya nafsi yangu mle, basi Mungu hawezi kuingia."

98 Hapo, jambo ndilo hilo, tu—tunamsonga anatoka. Tunamfukuza kwa ninii yetu. . .Kutoka kwa maskini kuliko wote kwetu mpaka aliye tajiri kuliko wote kwetu, kutoka kwa mdogo kuliko wote hata aliye mkuu kuliko wote, tunamweka Mungu nje ya maisha yetu kwa sababu ya nafsi zetu.

99 Nimesema mara nyingi, "Adui mkubwa kuliko wote niliye naye ni William Branham." Huyo ndiye anayemzuia Mungu. Ndiye mwenye kuzembea. Yeye ndiye anayefikia mahali wakati mwingine ambapo anawazia anaweza kufanya jambo fulani kulihusu, na, anapofanya hivyo, hilo linamsukumia Mungu moja kwa moja nje ya picha. Lakini ninapoweza kumwondosha jamaa huyo, ninapoweza kufikia mahali ambapo yeye ameondoka, basi Mungu anaweza kuja na kufanya mambo ambayo William Branham hajui kitu kuyahusu.

100 Hapo ndipo Mungu anapoweza kukutumia. Hapo ndipo anapoweza kumtumia yeyote wenu. Anaweza kumtumia mtu yeyote tunapoondoka njiani. Lakini mradi tumejiweka njiani, basi hatuwezi. Vema.

101 Sasa tunaona, jamaa huyu mashuhuri, Paulo, yeye alikuwa ni—alikuwa ni mtawala miongoni mwa wahubiri. Aliheshimiwa na kila dhehebu. Mtu huyo angalienda mjini na kufanya mkutano popote pale. Kwa sababu gani? Alikuwa na vitambulisho. Mbona, alikuwa ni mashuhuri sana, na ameyakinia kuwaponda-ponda watu wote waliokuwa dhaifu, hata akapata mamlaka kutoka kwa kuhani mkuu, mamlaka iliyo ya juu zaidi, kumfunga kila mmoja wa hao Wakristo. Mamlaka

ya kisiasa kutoka kwa kanisa lake, kuwafunga hao wote! Loo, alikuwa na nguvu! Angeweza kuwafunga Wakristo na kuwatupa gerezani kwa kuwa wasingekubaliana naye juu ya mafundisho yake ya kithiolojia, juu ya mafundisho ya Mafarisayo na Masadukayo. Yeye alikuwa akiwafunga Wakristo.

102 Lakini, angalia, ilimbidi kufungwa, yeye mwenyewe, apate kuzipoteza, aweze kupoteza nguvu zake na mamlaka. Akawa mfungwa, yeye mwenyewe, apate kupoteza kile kilichompa nguvu za kufunga nacho. Ilimbidi kupoteza kile alichokuwa, apate kufungwa.

103 Mungu huwapita waungwana! Aliwapita makuhani. Aliwapita wale waliokuwa na kiburi. Naye akamchagua Paulo, mtu huyu mashuhuri, na kumfanya aanguke mavumbini mwa nchi na kufanya mambo ambayo yeye. . . kama hao wengine waliyokuwa wakifanya. Aliwafanya watende katika . . . alimfanya atende kama wale aliokuwa akiwashika. Yeye alimfunga Paulo kwa Roho wa Mungu, kumweka huru kutokana na mamlaka aliyokuwa nayo kuwafunga Wakristo nayo. Ati waniambia Mungu hajui kile anachofanya? Yeye aliondoa nguvu zake kusudi apate kupoteza mshikilio wa—wake.

104 Ni wahudumu wangapi Mungu angeweza kuwatumia asubuhi ya leo kama wangemwacha tu Mungu awafunge kwa Neno Lake na kwa nguvu Zake, na kuwafungua kutoka kwa nguvu za madhehebu na mashirika! Ni watu wangapi waaminifu kwenye mji huu, asubuhi ya leo, wanaohudhuria makanisa haya makuu ya kimadhehebu, ni wangapi Yeye angeweza kuwajaza kwa Roho Mtakatifu, na kuiwasha moto nchi hii kwa Injili na nguvu, kama tu wangejichukua na kujifungua wenyewe mamlaka waliyo nayo na wafungwe kwa Roho Wake, wapate kuwa kama Paulo alivyokuwa, mtumwa wa upendo kwa Mungu!

105 Mungu alimchukua Paulo na kumfanya mtumwa, akamfunga Kwake na kumtuma kwa Mataifa ambao aliwachukia. Lakini, unaona, ilibidi afunguliwe kutoka kwa mamlaka yake ya kikasisi, apate kufungwa kwa nguvu za Mungu. Ilimbidi kupoteza nguvu zake na kuwa dhaifu na ovyo, kusudi apate kupokea nguvu za Mungu, apate kufungwa kwa Mungu, afanye yale Mungu angemwambia kufanya.

106 Hilo ndilo linalotupasa kufanya leo hii. Hilo ndilo ninalohitaji. Hilo ndilo kila mtu anahitaji, ni kupoteza utu wake, kupoteza uwezo wake, kupoteza kile alicho, apate kujitolea kikamilifu kwa Roho Mtakatifu. Mke nyumbani anahitaji hilo. Mvulana wa shule anahitaji hilo. Tunachukua. . . hata watoto wetu wadogo.

107 Mvulana fulani mdogo ninayewazia habari zake, jana alasiri ama juzi, ama siku moja, aliingia na kumfanya dada yake mkubwa kuandika somo lake upesi sana, kisha akaja na kuwaambia wavulana wadogo, kasema, "Whiu! Maswali

hayo yalikuwa ni rahisi." Mnaona, wanafundishwa, karibu, kudanganya.

108 Ingekuwa ni bora zaidi vipi . . . Na hao watu ni nguzo kwenye kanisa fulani. Ingekuwa bora vipi kwa Baba, asubuhi kwenye kiamshakinywa, kusema, "Yohana atafanya mtihani wake leo. Ee Mungu, kuwa pamoja na Yohana! Msaidie Yohana! Aliniomba kwenye chumba cha kulala asubuhi ya leo, akasema, 'Baba, niombee leo, sina budi kufanya mtihani wangu. Niombee.'"

109 Ni afadhali mvulana wangu angepata "F" nzu—nzuri, stahifu kwenye kadi yake, kufeli, kuliko mimi kujua alipata "A" dhahiri na kudanganyia. Naam, bwana! Tunachohitaji ni kujiachilia, kutegemea kabisa nguvu za Mungu.

110 Sasa, "kufungwa." Mungu huwapita waungwana na kuchukua udhaifu. Mungu huwapita wale wanaodhani wao ni kitu fulani, apate kumchukua mtu asiyejua kitu kusudi alitekeleze kusudi Lake maishani mwao. Hicho ndicho tunachopata.

111 Mungu alimwambia Paulo, "Uweza Wangu ni mtimilifu katika udhaifu wako. U—uweza Wangu huwa mtimilifu zaidi kadiri unavyokuwa dhaifu. Kadiri unavyoweza kujitolea Kwangu ndivyo ninavyoweza kukutumia. Kadiri unavyoweza kuisahau elimu yako, kadiri unavyoweza kulisahau dhehebu lako, kadiri unavyoweza kuusahau upuuzi wako na ujitolee Kwangu, ndivyo ninavyoweza kukutumia. Maana unapokuwa dhaifu, nita—nitalihuisha kusudi Langu Mwenyewe."

112 Mungu anaweza kufanya nguvu kutokana na udhaifu! Hiyo ndiyo sababu Yeye hufanya hivyo daima. Wakati alipowachagua wanafunzi Wake, ni nani angeweza kuwazia . . .

113 Unyenyekevu wa Mwanawe Mwenyewe wakati alipozaliwa katika hori, katika kibanda chenye samadi, katika zizi la ng'ombe, na akafungwa nguo za kitoto! Mnaona, Yeye angaliweza kupitia kwenye ikulu. Angaliweza kushuka kwenye ushoroba wa Mbinguni, na wote . . . gwaride kamili ya Malaika. Bali alichagua kumfanya Kristo Mfano wetu, kwa ajili yetu, ndipo akamleta katika unyenyekevu.

114 Kamwe hakumfunza katika shule za ulimwengu huu, bali Yeye alimfunza kwa Nguvu Zake Mwenyewe, kuninii . . . apate kujitolea Mwenyewe kikamilifu, sio kwa mawazo ya mwanadamu wala kwa nguvu za ulimwengu, bali kujitolea Mwenyewe kwa nguvu za Mungu.

115 Na hivyo ndivyo tulivyo leo, tunajitolea wenyewe leo katika madhehebu yetu makuu na milki. Tunajitolea kwa madhehebu, yale yanasema, yale *hayo* yanasema kuhusu jambo hilo. Bali hiyo ni kinyume na mapenzi ya Mungu. Inatubidi kujitolea kwa Roho wa Mungu na kwenda ambako Roho anasema twende. Hiyo ni kweli.

116 Waebrania wa Mungu ambao sisi. . .Askari wa Mungu, hasa, "mashujaa." Ndiyo kwanza tusome katika Kitabu cha Waebrania, mlango wa 11 na kifungu cha 34.

. . .*walitiwa nguvu baada ya kuwa* dhaifu, . . .

117 Ilibidi wawe dhaifu kabla ya kupata nguvu. Kutokana na udhaifu wao walitiwa nguvu. Ninyi mnaoyaandika Maandiko, huko nje, Waebrania 11:34. Vema.

118 Hili hapa jambo la kutufariji. Hili hapa jambo linalotia moyo. Kutokana na udhaifu na unyenyekevu Mungu huwachagua watu wa kuujenga Ufalme Wake kwao. Kama tukipata kwenda Mbinguni, kama tukipata kusimama Mbele za Mungu pamoja na Kanisa Lake, tutasimama katika kundi la watu ambao wamekuwa wanyonge na waliokataliwa na kutupiliwa mbali na ulimwengu, na wasiojua kitu.

119 Si ni ajabu kuwa Mungu alitufananisha na kondoo? Kondoo ndicho kitu kisichojiweza kuliko vyote kilichopo. Hakuna kitu kisichoweza kujihami kabisa kuliko kondoo. Sungura anaweza kukimbia; kuchakulo anaweza kupanda mtini; mbwa anaweza kuuma; simba anaweza kurarua; farasi anaweza kupiga teke; ndege anaweza kuruka; bali kondoo anasimama hajiwezi.

120 Na hivyo ndivyo Mungu anavyotutaka sisi. Tutambue ya kwamba hatujiwezi kabisa, ndipo Mungu anamchukua mtu huyo na kuanza kujifinyanga Mwenyewe ndani ya mtu huyo; kufanya mikono yake ifanye yale Mungu angetaka mikono ifanye, anaifanya midomo yake iseme yale midomo ya Mungu ingesema; kwa kuwa si yake, ni ya Mungu. Yeye anaanza kuumba utu, anaanza kuuchukua udhaifu huu na kujiumba Yeye Mwenyewe.

121 Yeye hutuleta hapa duniani, kwa kuwa basi. . .Sisi tuna elimu, sisi ni werevu. Hivi ulipata kuona nasaba, koo? Tunapochukua, kwa mfano, kama katika Habili, kutoka kwa Habili akaja Sethi; ukoo wa Sethi ulishuka moja kwa moja, ukafikia wakati wa Nuhu, wote hao walikuwa tu ni wakulima wanyenyekevu. Bali watoto wa Kaini walikuwa ni werevu, wajanja, wenye elimu, watu mashuhuri, wajenzi, weledi.

122 Lakini upande wa Mungu ulikuwa ni dhaifu na mnyenyekevu. Hivyo ndivyo Mungu alivyowatumia. Hiyo ni nafasi ya Mungu. Hiyo ndiyo njia ya Mungu ya kutufikia, ni wakati tukiwa wanyonge. Tunapata kitu basi. Hili hututia moyo, hakika, maana Ufalme wote wa Mungu umejengwa kutokana na watu wa namna hii. Ndipo unapofikia njia kama hiyo basi u— unaweza. . .umo katika Ufalme Wake.

123 Jambo ni kwamba, kwetu, kwamba. . .si kwamba sisi ni wanyonge mno, jambo ni kwamba sisi tuna nguvu nyingi mno. Tu—tu—tuna nguvu nyingi mno. Hivyo tu. Jambo ni kwamba tuna kichwa kigumu. Hiyo ni kweli, tuna nguvu sana kichwani mwetu. Tunajua mengi mno. Mungu anataka kuondoa hayo

kutoka kwetu. Hiyo ni kweli. Tuna nguvu nyingi mno, tuna nguvu nyingi mno hatuwezi kujitolea Kwake. Tunaninii . . . Tu—tunajitolea kwa nafsi zetu. Inatupasa kuwazia, "Vema, sasa, hapa, ni—nina akili ya kutosha kujua!"

124 Nilishangaa sana siku chache usiku zilizopita wakati mama alipokuwa ni mgonjwa, huko hospitalini. Nilienda kuninii . . . Kulikuwako na maskini mama mmoja kwenye mlango wa pili . . . Endapo maskini mama huyo yupo hapa, samahani, dada. Yeye ni maskini msichana wa Kentucky kutoka kule chini, nasi tulikuwa . . . na huyo alikuwa ni mama mkwe wake. Nami nilikuwa nikizungumza naye usiku huo, mimi pamoja na mke wangu, pale karibu saa saba usiku. Naye mume wake alikuwa amejilaza sakafuni akalala; akasema, "Ondoka hapa! Huna faida kwa mama yako, hata hivyo." Naye akamfukuza, mumewe, kutoka humo chumbani, kwa kuwa alikuwa amelala moja kwa moja kuegemea mlango ambapo manesi, hakuna mtu angaliweza kuingia; aking'orota tu, sakafuni. Kwa hiyo akamwamsha na kumfukuza.

125 Ndipo akaanza kuzungumza pale. Nikaanza kumzungumzia juu ya Bwana, na kadhalika. Naye akasema, "Vema," akasema, "yote niliyopata kujua ni jembe la shingo ya bata kwenye kishamba cha tumbaku, asubuhi na mapema, kung'oa magugu na kuvuta tumbaku, na kadhalika namna hiyo." Kasema, "Lakini, nakwambia," kasema, "baba alitupeleka, kila mmoja, shuleni." Kisha kasema, "Tungali hatuna akili."

Nikawaza, "Vema, labda hiyo ndiyo sababu."

126 Mnaona, hu—huna budi kuyaondoa mambo ya ulimwengu kwako. Sasa, mimi siungi mkono ujinga, si—sivyo, bali ninajaribu kuwazia unapofikia mahali ambapo unafikiri ya kwamba unaninii tu—unajua tu mengi sana hata hakuna mtu mwingine anayejua lolote kulihusu. Maarifa yako ni sawa mradi tu hayaninii—hayaitatizi ahadi ya Mungu.

127 Tunatawaliwa na hisi tano, na hizo hisi tano (kuona, kuonja, kugusa, kunusa, na kusikia) ni sawa kabisa mpaka zinapokatiza hisi ya Imani. Ndipo zinapopingana na Imani . . . Na unajuaje ni ipi iliyo sahihi? Kwa sababu Imani daima itakubaliana na Neno. Halafu kama—kama imani yako ni kinyume na Neno, ama unafikiri ni kinyume, basi huna Imani. Una imani ya kujisingizia. Una kiburi katika hisi zako, cha kisomo ambacho umesomea, ama chochote kile. Lakini unapoondokea jambo hilo na unategemea Imani kabisa, nayo Imani inaweza tu kujengwa juu ya Neno la Mungu (Imani sahihi).

128 Daktari fulani aliniambia wakati mmoja, kasema, "Ninaamini, Billy, kama hao watu . . . kama ungewaambia watoke waende huko nje na kugusa ile nguzo, ule mti, nao waliamini ya kwamba watapona, wangepona vivyo hivyo."

129 Nikasema, "La, bwana. Haiwezekani, daktari, kwa sababu ya jambo hili moja, unaona, hao watu wanajua ya kwamba hiyo ni nguzo tu. Wanajua hamna uweza wala nguvu kwenye ile nguzo."

130 Lakini mtu yeyote aliye na akili timamu angejua ya kwamba hilo ni Neno la Mungu aliye hai, kwamba ninaweza kuwekea msingi imani yangu juu ya hilo na nijue ni BWANA ASEMA HIVI! Na kama chochote ni kinyume cha Hilo, basi siamini hisi zangu. La, bwana, achana nazo tu. Tumia ile hisi yako nyingine, hisi ya Imani.

131 Vema, Mungu huwachukua watu hao kufanya. . . Wakati wakiwa ni duni, watajitolea Kwake.

132 D. L. Moody wa Chicago, alikuwa wa Boston, alikuwa ni fundi wa viatu; maskini jamaa mdogo, asiyejiweza, hakujitegemea. Sasa, hebu chukua shule hizi kuu walizo nazo, ile Shule ya Moody huko juu, kama Dwight Moody angalifufuka tena na kuona shule hiyo, jambo la kwanza Dwight Moody angefanya ni kuiondolea mbali shule hiyo.

133 Kama Martin Luther angalifufuka, jambo la kwanza angalifanya ni kuondolea mbali dhehebu la Kilutheri. John Wesley angefanya vivyo hivyo. Hao watu kamwe hawakuanzisha madhehebu hayo, ni watu waliowafuata, ndio walioyaunda.

134 Paulo kamwe hakuundia kanisa lolote dhehebu, kwa sababu alisema, yeye mwenyewe, "Baada ya kuondoka kwangu, wengi wa umati wenu wenyewe watainuka miongoni mwenu, wakisema mambo mapotovu." Ilikuwa ni baada ya kifo cha Paulo, na miaka mia moja (ama mbili) baada ya hapo, ndipo walipounda kanisa Katoliki, dhehebu la kwanza.

135 Watu waliinuka! Ilikuwa ni baada ya kifo cha Moody ndipo walipojenga Shule ya Moody; baada ya kifo cha Wesley ndipo walianzisha kanisa la Wesley; baada ya kifo cha Luther ndipo walianzisha kanisa la Luther. Mungu hutuma mashujaa; nao wanajenga. . .

136 Si ajabu Yesu alisema, "Enyi—enyi kuta zilizopakwa chokaa!" Akasema, "M—mnayapamba makaburi ya manabii, nanyi ndinyi mliowaweka mle!" Hiyo ni kweli.

137 Watu hawa mashuhuri waliinuka; ndipo wakawajengea kumbukumbu. Nafikiri, kama tu vile Daudi, "Alimtumikia Mungu vema katika kizazi chake." Kwa hiyo hiyo ndiyo njia ya kufanya jambo hilo. Kuyaacha madhehebu na mambo mengine pale, ambayo unayaweka mbali nawe.

138 Moody, maskini fundi wa viatu, alikuwa ni dhaifu. Yeye alikuwa ni mfano wa udhaifu. Jambo la kwanza inasema ya kwamba Moody alifanya. . . Hakuwa na elimu hata kidogo, nayo sarufi yake ilikuwa ni mbaya sana ilikuwa ni ya kuchukiza sana. Mtu mmoja alimjia wakati mmoja na kusema, "Bw. Moody,"

kasema, “sarufi yako ndiyo mbovu sana niliyopata kusikia maishani mwangu.”

139 Akasema, “Ninawaongoa watu kwa ujinga wangu, je! unafanya nini na elimu yako?” Nafikiri hilo lilikuwa ni jibu zuri. Hakika lilikuwa zuri!

140 Na sasa, ukiwa mwanafunzi wa Shule hiyo, bila shaka itakubidi kuwa msomi hodari. Hiyo ni kweli. [Ndugu mmoja anasema, “Waliigeuza tu!”—Mh.] Sasa, naam, ni kweli “waliigeuza tu,” wakaenda moja kwa moja upande huo mwingine.

141 Hivyo ndivyo watu wanavyofanya. Wakati niliposema mwanzoni mwa ujumbe wangu...Badala ya Wakristo kujinyenyekeza na kujifanya tupu wapate nafasi zaidi kwa ajili ya Mungu, wanajaribu kujijenga wenyewe kwa maarifa ya kujibunia, ama maarifa fulani ya shule ya ufundi, ama kitu fulani, kinachowapeleka mbali zaidi na Mungu kuliko walivyokuwa wakati walipoanza.

142 Hilo ndilo ninalowazia juu ya miito hii ya kujibunia ya madhabahuni. Unamwingiza, ndipo wakati huo mwingine ni vigumu mara kumi zaidi kumrudisha tena. Acha aketi na kusikiliza mpaka Mungu amfanyie jambo fulani! Halafu hebu aje na kukiri hilo, na kuinuka, akiliitia Jina la Bwana. Hiyo ni kweli.

143 Mwangalieni Moody, dhaifu katika elimu, dhaifu katika hotuba, alitoa mlio wa farasi kwa pua yake. Nilikuwa tu nikisoma historia yake hivi majuzi, “Alitoa mlio kama wa farasi kwa pua yake, ugonjwa wa mapua.” Kimwili ni mdogo, jamaa mwenye upara, masharubu yakining’inia kwenye ninii yake...?...; maskini, jamaa mdogo, mfupi. Kimwili, alidumaa. Kwa hiyo hakuwa na kitu ila udhaifu daima. Bali Mungu alimtumia kuutikisa ulimwengu katika siku yake!

144 Wakati mmoja kulikuwako na mwandishi wa habari aliyeenda kwenye mkutano wake (nilikuwa nikisoma), na waandishi wa habari, kutoa habari kwamba huyu alikuwa ni mtu wa namna gani (mtu mashuhuri, jamaa mkuu).

145 Iko wapi ile swichi ndogo mnayozifunga kanda kwayo? Ndiyo hii? Itanibidi tu kushikilia hilo hapo.

146 Mtu ma—mashuhuri, Moody alikuwa hivyo. Alikuwa ni mtu mzuri. Na kwa hiyo angeweza kuuvutia usikivu wa watu, kuwavutia kwa usemi hodari. Kwa hiyo alitokea mwandishi wa habari aliyemwendea Bw. Moody na kusema...aliyeenda mkutanoni akatoe habari kwamba ni ongezeko kubwa la jinsi gani...

147 Kama vile mwandishi mwingine alienda na kutoa habari juu ya mwinjilisti mwingine mashuhuri, hivi majuzi, kasema, “Mtu huyo ana ushawishi wa maneno. Yeye ni Daktari wa Uungu.

Anatumia sarufi iliyo bora kuliko zote nilizopata kusikia. Yeye huwashika watu katika saikolojia yake. Anaweza kuwashikilia watu kwa ushawishi mkuu."

148 "Dwight Moody," wakati huyo mwandishi alipoenda, alisema, "Sioni kile kilicho ndani yake cha kumvutia mtu yeyote." Kasema, "Jambo la kwanza, ana sura mbaya awezavyo kuwa. Jambo la pili, kimwili, ana sura mbaya. Jambo jingine" akasema, "yeye ni, hana elimu. Sarufi yake ndiyo mbovu kuliko zote nilizopata kusikia!" Kisha kasema, "Ana sauti ya farasi na anaforota wakati akihubiri." Kisha kasema, "Sioni kitu katika Dwight Moody kingaliweza kuvuta usikivu wa mtu yeyote."

149 Bw. Moody aliletewa makala hiyo. Akaisoma, akajichekea, kasema, "La hasha; ni Mungu. Hakika! Watu hawaji kumwona Dwight Moody, wanakuja kumwona Mungu."

150 Watu hawajali ni kiasi gani unashuhudia, wanataka uhalisi fulani pale katika maisha yako unaothibitisha kwamba Mungu amekushika. Hata uwe Mmethodisti, Baptisti, Pentekoste, yeyote uliye, wao wanataka kumwona Mungu. Hiyo ni kweli, watu wa...watu mashuhuri, watu walio dhaifu na wanautambua udhaifu wao.

151 Mwangalieni Musa, yule kijana msomi. Loo, yeye alikuwa ni mwanazuoni. Alikuwa amefunzwa katika hekima yote ya Misri hata angewafundisha Waebrania. Angeweza kuwafundisha Wamisri. Angeweza kumfundisha mtu yeyote, kwa kuwa Musa alikuwa ni mtu mashuhuri, mtu mwerevu. Loo, alikuwa ni mtu mwenye nguvu.

152 Katika wazo la Cecil DeMille la jambo hilo, wakati—wakati alipoonyesha *Zile Amri Kumi*, basi alimfanya mtu huyu kuja aliyekuwa...ninasahau jina la mtu huyo aliyeicheza sehemu ya Musa mle ndani, mwigizaji fulani, bali ni mtu mkubwa mno mwenye mikono mikubwa na nguvu. Na Musa labda alikuwa ni mtu wa aina hiyo.

153 Tunajua yeye alikuwa mwenye nguvu na aliyefunzwa vizuri, kwa hiyo alijichukulia mwenyewe, akiiona haja ya siku hiyo. (Lo, Mungu na ajalie hili lizame kabisa!) Akiiona haja ya siku hiyo, Musa akiwa na nguvu zake za usomi na kipaji chake alichotumia...Alikuwa ni mtu mwerevu. Alikuwa ni halifa wa Farao. Alikuwa na saikolojia. Alikuwa na—alikuwa na mamlaka. Alikuwa na nguvu za kimwili. Alikuwa na—alikuwa na kila kitu. Kwa hiyo akasema, "Nimejihami sawasawa. Ninajua yote hayo. Na kama yupo mtu nchini aliye na uweza wa kulifanya, ni mimi. Kwa hiyo, mimi ndimi mtu wa majira haya kwa hiyo nitatoka nje." Naye akatoka akaikamilishe kazi iliyokuwa ni ya kweli na katika mapenzi ya Mungu, naye akatoa vipaji vyake vya kimaumbile. Naye Mungu akavikataa! Asingetumia hata kitu kimoja alichokuwa nacho Musa.

154 Asingeweza kukitumia wakati huo, wala Yeye. . . wala hawezi kukitumia sasa. Mungu hawezi kutumia vipaji vyetu vya kimaumbile. Inatupasa kujiondoa njiani pamoja na vipaji vyetu, na kujitolea kwa mapenzi na uweza wa Mungu.

155 Wasema, "Vema, ndugu, ninaweza kuhubiri." Yeye hawezi kutumia hicho mradi tu *wewe* unaweza kuhubiri. "Hiyo ni sawa, ninaweza kufanya *hiki*, ninaweza kufanya *kile*." Huwezi kufanya lolote. Vema, basi Mungu hawezi kukitumia. Bali kama utajitolea kwa Mungu na kumwacha afanye jambo hilo!

156 Unasema, "Vema, Ndugu Branham, ninajua. Mimi ni mwalimu." Vema, mradi tu *wewe* ndiye mwalimu, mbona, Yeye hatafika mbali sana. Bali Roho Mtakatifu ndiye Mwalimu wetu. Hakika, ndivyo alivyo! Mungu alimtuma Roho Mtakatifu apate kuwa Mkufunzi juu ya Kanisa.

157 Watu wengine huenda shuleni kwa miaka na miaka na miaka. Wanafanya nini? Wanasoma makala kutoka kwenye Chumba cha Juu, na kwa hiyo (loo, hilo ni zuri) unachukua somo la Kitaifa la shule ya Jumapili. Sina neno dhidi ya hilo. Hayo ni Maneno ya Mungu, na kadhalika, bali yamewekwa pamoja na wenye akili! Yanapaswa kutokana na nguvu na kufufuka kwa Kristo, na huwezi kuvitegemea vipaji vyako vya kimaumbile.

158 Kwa hiyo, Musa, hili jitu zuri, kijana, lenye nguvu, mtu mwenye akili, aliondoka kwenda kufanya kazi nzuri; bali Mungu kwa urahisi, kabisa asingeweza kumtumia. Asingeweza kutumia vipaji vyake vya kimaumbile.

159 Na sisi hatuwezi. . . Si leo hii, ambapo hatuwezi. . . Mungu hawezi kutumia vipaji vyetu vya kimaumbile.

160 Lakini kuna jambo moja alilokuwa nalo Musa ambalo ninalipenda, yeye alikuwa na akili ya kutosha kujua ya kwamba alikuwa ameshindwa. Sisi hatuna. Hivyo tu. "Tutajiundia dhehebu *jipya*. Tutampata mtu mwingine mwenye karama ya uponyaji, ama chochote kile," Wapentekoste, mnaona. Mnaona? Ha—hatujui tu vya kutosha kujua ya kwamba tumeshindwa. Kanisa la Kipentekoste, Assemblies of God, United, hayo mengine, inaonekana kana kwamba hawana uwezo wa kujua ya kwamba wameshindwa. Haleluya! Loo, laiti ningeweza kulifanya hili lishike. Wameshindwa. Dhehebu la kanisa limeshindwa! Kama tu vile Marekani imeshindwa, inatetemeka na kuogopa, na mabomu yakining'inia kule kwa ajili yao, wanajua wamecheza dansi kwelikweli na kuyaingiza maisha yao kuzimuni. Nao wameshindwa, Roho ameondoka kwao. Ingekubidi kuichambua miti kupata vijana wa kupelekwa jeshini; wameona kile kilichowapata hao wengine. Tumeshindwa! Kanisa limeshindwa. Wanajua hilo.

161 Musa alitambua hilo, naye alijua vya kutosha wakati huo. . . Mungu alimchukua akampeleka huko nyuma, nyikani, kumfundisha udhaifu wa kibinadamu. Alimpeleka huko

akamfundishe yote kuhusu hayo. Kajifunza vizuri sana! Loo, jamani, alipata somo kwelikweli! Hapana shaka Mungu alikuwa na wakati mgumu pamoja naye huko nyuma! Mwajua, Musa alikuwa na hasira; na Mungu akampa mke jina lake Sipora, alikuwa nayo, pia. Kwa hiyo ninawazia kila kitu hakikuwa ni cha kupendeza huko nyuma upande wa nyuma wa jangwa kwa kitambo kidogo, wakati hasira zao wawili zilipolipuka kwa pamoja.

162 Nadhani wazo lake la kielimu jinsi saikolojia inavyopaswa kumdhibiti mtu halikufaa sana, kwa sababu, wakati alipokuwa njiani kuelekea Misri, ninaona Sipora angali alikuwa na hasira. Aliikata govi ya mwanaye na kuibwaga mbele ya Musa, kasema, "Wewe u bwana wa damu kwangu mimi."

163 Naye Mungu alikuwa na hasira sana naye akaninii... akamtafuta kwenye mkahawa, kama angalimpata angalimwua. Nadhani kuna mambo madogo yaliyombidi Mungu kumfundisha huko nyuma, mnaona, kwamba yeye alikuwa ni mwanadamu. Hekima yake yote ya Misri na nguvu zake zote za kielimu, Mungu asingeweza kutumia moja ya hizo.

164 Unakuja, unasema, "Sasa, Bwana, nimeelimishwa kwa miaka arobaini sasa, mimi ni—mimi ni mwanafunzi mwenye akili. Ninaweza kuinukuu Biblia hiyo huku nimeyafunga macho yangu." Mungu hawezi kutumia hata kidogo cha hayo. Unaona? La.

165 "Loo, mimi ni mfuasi wa kanisa lililo kubwa kuliko yote nchini. Mimi—mimi ni ninii...Mimi ni *hili*, Bwana. Loo, mimi ni Mpentekoste. Mimi...Utukufu kwa Mungu! Ndio kwanza nimpokee Roho Mtakatifu hivi majuzi usiku. Haleluya! Utanifanya nifanye *ninii*." Mungu hawezi kutumia hayo hata kidogo. La!

166 Wakati wowote unaposhindwa na unatambua umeshindwa, na kisha urudi na kujinyenyekeza. Kuwa dhaifu, pata kujua wewe ni mwanadamu. Na hakuna chochote cha elimu yako kinachoweza kuninii...Udhaifu wa kibinadamu kamwe hautatumiwa na Mungu; Mungu kwa udhaifu wa kibinadamu hujimimina Mwenyewe ndani yako, kisha anajitumia Mwenyewe. Unakuwa tu chombo. Hakika! Huna budi kujiondoa njiani.

167 Musa, loo, yeye alijifunza, alijifunza udhaifu wa kibinadamu vizuri sana. Alijifunza vizuri sana, mpaka, Mungu alipomwita, yeye alikuwa na udhaifu saba ambao angeweza kuubishania wito wa Mungu. Uliwahi kusoma katika sehemu ya kwanza ya Kutoka, ule udhaifu saba? Ni—nimeuandika hapa. Ninataka muusikilize. Udhaifu wa kwanza aliokuwa nao ulikuwa ni ukosefu wa ujumbe. Udhaifu wa pili aliokuwa nao ulikuwa ni ukosefu wa mamlaka. Udhaifu wa tatu aliokuwa nao ulikuwa ni

ukosefu wa ufasaha. Wa nne ulikuwa ni marekebisho. Wa tano ulikuwa ni ufanisi. Na wa sita ulikuwa ni kukubalika.

168 Sasa, hebu linganisha wako na wake uone kama unaweza kutokea na huo, uone kama unaweza kuwa dhaifu kama alivyokuwa. "Bwana, mimi—mimi sifai kitu. Siwezi kuzungumza. Ni—ni—nilimwua Mmisri. Siwezi kurudi. Loo, kila kitu! Hawatanipokea. Sina ujumbe wowote. Nina-. . . Siwezi kuzungumza. Na mimi si—mimi si mwepesi wa kunena." Na mnaona jinsi alivyokuwa? Hakuwa kitu! Ndugu, alikuwa ameponywa. Naam, Mungu angeweza kumtumia basi baada ya kuponywa. Mnaona? Naam.

169 Naam, Yeye anaweza kututumia baada ya kuponywa, kuona kwamba "Ph.D. yangu na LL.D. na L.D. maradufu," ama chochote kile, "digrii zangu zote si kitu." Mungu hawezi kuzitumia!

170 "Vema, mimi ni Assembly of God. Mimi ni wa Umoja. Mimi ni Mbaptisti. Mimi ni Mpresbiteri." Mungu hawezi kutumia hayo hata kidogo! Kadiri utakavyotoka humo upesi, vema, ndivyo wewe—uta—utakavyokuwa bora zaidi kuji—kujitolea kwa Mungu.

171 Kama vile nabii alivyokuwa, kasema, "Mimi ni mtu mwenye midomo michafu, na miongoni mwa watu wachafu." Ndipo Malaika akaondoka akachukua ma—makoleo, akaenda hadi madhabahuni akatwaa kaa la moto na kuigusa midomo yake. Ndipo akasema kwa sauti kuu, "Bwana, mimi hapa; nitume mimi." Naam, baada ya kutambua ya kwamba yeye. . .Ingawa alikuwa ni nabii, yeye alikuwa na midomo michafu.

172 Mara tunapoweza kutambua ya kwamba sisi si—sisi si kitu, kwamba wewe si kitu, wewe ni mavumbi ya nchi. . .Mungu hawezi kukutumia. . .Naam, ujuzi wako. . .Udhaifu wako wote usingeweza kulinganishwa na wa Musa. Yeye alikuwa na udhaifu sita mbalimbali hapa, naye alikuwa amejua udhaifu wa kibinadamu.

173 Sasa angalia tofauti kati ya *huyo* Musa akikutana na Mungu, na *Musa* akiangalia kwenye. . .?. . .kama leo hii. Kasema, "Aisee, tunahitaji *ninii*! Tunahitaji uamsho nchini. Nitakwambia kile nitakachofanya, ninarudi nikasome mpaka nitakapopata Digrii yangu ya Sanaa. A-ha! Ninarudi nikasome mpaka nitakapowekwa wakfu kama LL.D. Nitasoma fasihi. Nitafanya yote haya, ndipo nitatoka nje na nitakuwa 'mtu wa majira haya.' Nitawafunika jamaa hawa wote ambao wameanzia huku." (Loo, ndugu!) "Nitajipatia jengo la dola milioni tatu. Nitajipatia kadilaki dazani moja. Na. . ." Loo, ndugu! Afadhali—afadhali hata usianze, maana kwanza umeshindwa, unaona. Lakini shida yake ni kwamba wao hawajui hilo!

174 Wanadhani inakubidi kuwa na nywele zilizotiwa mawimbi na kuvaa koti maalumu na kusema "aa-mina" vizuri sana,

na yote namna hii, na kuwa mtawala. Huyo ni kibaraka cha mwanamke!

Mungu anawataka wanaume, wanaume watauwa, wanaume wanaoweza kutikisa!

175 Lakini leo hii tunataka Hollywood. Tunataka kitu ambacho—ambacho kinapendeza jicho. Tunataka kitu kinachoweza kuzungumza kielimu sana hata anaweza kutuacha tulale dakika tano wakati akininii . . . Jumapili asubuhi.

176 Mungu anataka watenganishi watakaomrusha kama mwali wa radi, ahukumu dhambi hata kwenye mizizi, (hiyo ni kweli) aichimbue.

177 Lakini tunaninii . . . Tunawataka wachungaji wetu wa kielimu. Watu wengi wanamtaka mchungaji wa kunong'oneza, mtu anayesema, "Naam, kipenzi."

Mungu anataka radi! Naam, bwana.

178 Kuwapigapiga mgongoni, na hizo nywele fupi na wamejipaka vipodozi, na chochote kile, na kuvaa nguo ambazo walimwagiliwa ndani, na yote namna hiyo, wala wasiseme neno dhidi yake.

179 Mtu mashuhuri aliniita ofisini mwake hapa, (si ofisi yake) ofisi ya huduma yake, hapa muda si mrefu uliopita, kasema, "Ninataka kukuwekea mikono upate kuachana na hayo!"

Nikasema, "Usifanye hivyo. Usifanye hivyo. La, bwana."

180 Unapokomesha hayo, unaukomesha Ujumbe. Unamkomesha Mungu unapofanya hivyo. Naam, bwana. Hatutaki yoyote ya hayo.

181 Hivi Mungu alimwonea Musa huruma kwa udhaifu wake wote, kasema, "Maskini Musa, jambo fulani—jambo fulani hakika limekupata, ulianguka kutoka kwenye digrii yako. Loo, jamani! Hapa, naam, ulikuwa mtu mashuhuri, mwenye elimu, na hapakuwapo na kitu kingalikuzuia. Ndugu, ulikuwa na Ph.D. na LL.D. zako zote, na chochote kile, na sasa hapa unakuja ukikiri kwamba wewe si kitu, huwezi kufanya kitu. Wewe ni—wewe ni dhaifu sana"? La! Mungu hakumwonea huruma. Mungu hakumhurumia. Mungu alimponya na upuuzi wote huo wakati huo. Hakumhurumia.

182 Lakini tunaona, kama unaliandika, Kutoka 4:14, "Hasira ya Mungu iliwaka dhidi yake." Mungu hakumhurumia kwa sababu alikuwa ni dhaifu.

183 Unasema, "Ee Bwana, ninajisikia vibaya sana, siamini ningeweza kufanya jambo hilo." Mungu hakuhurumii; anajisikia kama kukupiga teke kidogo. Unaona? Unaona? Hakika. Mungu hakuhurumii; a—anakukasirikia. Unafikia tu kiwango ambapo anaweza kukutumia. Naam.

184 Musa akiponywa, Mungu anaweza kumtumia. Yeye alikuwa na dawa, alikuwa mbali na uweza wa kibinadamu wakati huo. Hakuwa na kitu angaliweza kutegemea wakati huo, maana a—alikuwa tayari basi kwa ajili ya huduma.

185 Mungu alisema, "Miaka arobaini hapa nje nimekufanya wewe na Sipora kugombana na kuzozana huku nje kwenye nyika hii, kama ungeweza kujua kama kulikuwako na udhaifu wa kibinadamu ama hakukuwako, ambapo unasimama huku juu kama mtawala mkuu, 'Aloo, Daktari Musa. Habari za asubuhi, Kasisi, Bwana. Naam, bwana. Musa, wewe ndiye mtawala ajaye. Wote. . . Sote tunakuwazia.' Sasa uko huku nje jangwani pamoja na kundi la kondoo na mke mwenye hasira." Mnaona? Hilo lilimponya. Naam, bwana. Musa akiwa katika hali mbaya sana, bali Yeye alisema, "Sasa ninaweza kukutumia, unapotambua ya kwamba wewe si kitu. Sasa njoo huku karibu na kichaka hiki kinachowaka moto, ninataka kukutuma huko." Loo, jamani!

186 Mungu, tupe wengine zaidi wa aina hiyo, tupe wanyonge wengine. Hao ndio tunaohitaji, wanyonge. Hakika!

187 Ilikuwa ni Yakobo, mwajua. Yakobo alidhani alikuwa ni jamaa mashuhuri wakati mmoja, mwajua, angeweza kudanganya tu na kuepuka chochote kile. Alitoka akaenda akaweka fito za mpopla ambapo kondoo na ng'ombe za baba mkwe wake wakati walipokuwa na mimba, na kuwageuza kuwa kondoo wenye milia, na kuzitupa namna hiyo wakati walipoenda kunywa maji. Na, muda si muda wajua, Yakobo akawa mtu mashuhuri. Hakika. Alikuwa ninii. . . "Kweli aliitwa *Yakobo*, hapana kosa," Esau alisema, "yeye alikuwa 'mdanganyifu' kweli." Kwa hiyo alikuwa ni mdanganyifu. Alikuwa akiendelea vizuri, akipata faida, alikuwa na makundi makubwa na wake na kondoo na ng'ombe na maksai, na—na kila kitu, alikuwa na kila kitu.

188 Lakini usiku mmoja (loo, jamani!) wakati aliposhuka kwenye kijito kidogo wakati mmoja, alikuwa akitaka kukivuka, alifikia mahali ambapo Malaika alimshika. Ndugu, maskini Yakobo alishikilia usiku kucha. Hakika alishikilia muda mrefu. Bali wakati alipojisalimisha, wakati alipodhoofika wala asingeweza kushikilia zaidi. . .

189 Ee Mungu, jalia kanisa liwe namna hiyo, lifikie. . . kanisa lifikie mahali ambapo lisingeweza kushikilia zaidi kwa vipaji vyake vya asili, bali halina budi kujitolea kwa Mungu. Hebu Wamethodisti wajionee aibu kwamba wao ni Methodisti. Hebu Wabaptisti na hebu Wapentekoste wajionee aibu, na waache kushikilia, na wajitolee kwa Roho.

190 Hapo ndipo Yakobo alifanyika "mtawala wa Mungu." Biblia ilisema ya kwamba alifanyika "mtawala," na jina lake likabadilishwa. Unaona? Na—na, kumbukeni, yeye alikuwa mtu mashuhuri mwenye nguvu upande *huu*, mwenye nguvu

kiakili; bali upande *mwingine* yeye alikuwa ni mtawala anayechechemaa, mnyonge na amedhoofika sana, bali alikuwa na nguvu mbele za Mungu.

191 Naam, huenda ukaninii . . . Dhehebu lako huenda likavunjika vipande-vipande. Sifa zako katika ujirani, huenda ukawa "kunguru wa mtindo wa kale" tangu hapo na kuendelea, katika ujirani. Hilo laweza likawa ni sawa. Lakini nitakwambia, utakuwa na nguvu kwa Mungu. Afadhali niwe namna hiyo. Nitashika njia hiyo wakati wowote.

192 Wanafunzi walirudi wakishangilia kwa kuwa walikuwa na furaha ya kwamba walihesabiwa kuwa walistahili kubeba dhihaka kwa ajili ya Huduma hiyo na kwa Yesu. Hakika! Watakuita "mtakatifu anayejifingirisha."

193 Ondoka mahali hapo wakati mmoja, hebu pavunjiliwe mbali. Jiachilie kutoka kwa ninii yako, "Vema, aisee, Mimi ni Mmethodisti," ama "Mpresbiteri" ama "mimi ni Assemblies," "Mimi ni Umoja, mimi ni mwema tu kama ulivyo wewe." Vema. Hebu ondoka tu humo wakati mmoja, jiachilie. Chukua yote . . .

194 Hebu malaika akushike wakati mmoja, malaika wa Bwana atakayekuletea Ukweli wa Ujumbe. Acha akushike wakati mmoja, utanyenyekea hata kufikia ubatizo katika Jina la Yesu, utanyenyekea hata kufikia Hilo lingine lote. Naam, utanyenyekea, hakika utanyenyekea. Naam, uta—utasahau tu kisomo hiki chote.

195 Siku chache zilizopita, mmoja wa marafiki wazuri sana nilio nao, mtu mzuri, aliniambia, nikiondoka chumbani baada ya kuwa kwenye mahojiano, nikaondoka chumbani, kasema, "Ndugu Branham . . . " Na mtu huyu amekuwa mmoja wa wadhamini wangu kifedha kule mkutanoni. Nikafika mahali ambapo sikujua jinsi nitakavyoyaendeleza mambo, nikimtumaini Mungu tu; mtu huyu angezilipia zote. Naam, mtu mzuri tu! Ndipo mtu huyu akafanya safari akaja kutoka kwenye jiji kubwa, hapa siku chache zilizopita usiku, akasimama chumbani na kuniambia jioni moja, kasema, "Ndugu Branham," kasema, "ninataka tu kusema jambo moja." Kasema, "Hakuna mtu nimjuaye ila ambaye anakupenda."

Nikasema, "Ninafurahi sana kwa jambo hilo."

196 Kasema, "Ndugu Branham, kuna jambo moja tu, jambo moja kasoro."

Nikasema, "Ni lipi hilo, dada?"

197 Kasema, "Vema, jambo pekee ndilo hili, Ndugu Branham, ya kwamba kama ungepatana tu kidogo juu ya Fundisho ulilo nalo," kasema, "kila dhehebu lingekupokea."

198 Nikaona papo hapo, nikawazia . . . Nikasema, "Ni Fundisho lipi, dada?"

Na akasema, "Loo, huo ubatizo katika Jina la Yesu."

199 "Loo!" Nikasema, "Lakini, dada, usingeweza kutarajia nipatane juu ya Neno la Mungu na ningali niwe ni mtumishi wa Mungu."

200 Na akasema, "Vema, hapa, lipo kundi la wahudumu ambalo niko hapa kuliwakilisha la jiji hili kubwa." Kasema, "Iwapo utawaambia ya kwamba Malaika wa Bwana anayekupa maono haya alikwambia ukabatize katika Jina la Yesu, basi wako tayari kuukubali."

201 "Vema," nikasema, "ujuzi wao ni dhaifu kuliko maji yaliyooshewa vyombo!" Nikasema, "Sijali yale malaika yeyote angesema, kama si kulingana na Neno siliamini!" Nikasema, "Kama huyo malaika aliniambia jambo fulani tofauti na Hilo, nisingemwamini malaika huyo." Kweli! Neno la Mungu ndilo la kwanza, juu ya malaika wote na kila kitu kingine! Malaika wa kweli . . . Nikasema, "Kama hakuniambia Hilo, nisingemsikiliza." Naam.

202 Mama huyo hakujua la kufanya. Akasema, "Kamwe sijasikia kitu kama hicho. Sikujua Hilo." Mnaona, haya basi. Kwa hiyo nikampa maskini mama huyo Maandiko fulani. Naye akasema, "Ninarudi moja kwa moja nyumbani na kulisoma Agano Jipya. Sijapata kulisoma." Mnaona, haya basi. Loo, jamani! Loo, jamani! Hapo ndipo unapofikia. Loo, jamani!

203 Achana na kujaribu kushikilia. Achilia! Hilo ndilo unalotaka kufanya: kuachilia. Yakobo, wakati alipoachilia alikuwa ni sawa, alifanyika mtawala na alikuwa na nguvu na Mungu.

204 Alikuwa ni *maskini* Daudi amevaa koti lake la kikasisi la Sauli, aliyeondoka kwenda ku—ku—kupigana na Goliathi. Ndipo wakati Daudi alipoanza kwenda kule kupigana na Goliathi huku amevaa silaha hizi zote kubwa, aliangalia kote, akaangalia nyuma, alionekana kama hao wengine, kwa hiyo akasema, "Kuna kasoro fulani hapa."

205 Mradi tu unafanana na ulimwengu na kupatana na ulimwengu, na kufanya jambo lile lile wanalolifanya walimwengu, kuna kasoro fulani.

206 Daudi akasema, "Hii inaonekana imezingirwa sana. Nina Digrii ya Udaktari, nina Ph.D. Mnaona, mimi ni mfuasi wa dhehebu kubwa, ningewezaje kwenda kupigana na vitu hivi vyote? Sijui neno kuvihusu. Sijui neno kivihusu!" Daudi akasema, "Nivueni vitu hivi." Hiyo ni kweli. "Kama ninaenda kupigana kwa ajili ya Mungu sitaki kuonekana kama kundi hili la hawa waoga wanaosimama hapa, wote wamevaa silaha na kujifunga. Siwezi kufanya mkutano . . . "

207 Mikutano mingi, watu wengi, wahudumu wengi wanaonijia na kukiri kwamba wanaamini kwamba ni sawa kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, bali wanasema "Dhehebu letu lingetutupa nje." Ewe udhuru dhaifu! Jivue silaha za Sauli!

208 Nipe nguvu na uweza wa Roho Mtakatifu! Mungu, nitume na kombeo, haidhuru ni nini (ni dogo vipi), nikamwangushe adui. Hiyo ni kweli. Nitume, bali usiniache nivae kama hao wengine kwa L.L., Ph.D., Madaktari, upuuzi wote wa namna hiyo.

209 Daudi alisema, "Kitu hiki hakionekani sawa." Akasema, "Sijui lolote juu ya hicho." Akasema, "Jambo pekee nijualo, nililo nalo ambalo naninii . . . Huko nyuma upande wa nyuma wa jangwa nilikuwa nikiwachunga kondoo wa baba yangu." Kisha kasema, "Simba aliingia akamnyakua maskini mwana-kondoo huyo na kutoroka naye, nami nilijua huyo alikuwa ni mwana-kondoo wa baba yangu, na, loo, ni—ni—ninaninii . . . Sikuwa na silaha, bali nilichukua tu kombeo langu na kumfuata." Kasema, "Nilimwua na kumrudisha mwana-kondoo." Loo, jamani! Hao waliosimama pale, mkuki mkononi mwao, wasingeweza kufanya hivyo.

210 Hiyo ndiyo shida ya siku hizi. Mungu ana kondoo wengi sana waliopotea, madhehebu na kadhalika yamewaiba, wakawaingiza kwenye saikolojia. Mungu tupe Daudi wenye Neno la Mungu na nguvu za Mungu, kulielekeza tunapoenda kukabiliana na majitu haya yenye elimu (Kweli!) wakiwa na Ph., LL.D., Q.U.S.T zote, ama chochote kile. Nipe Neno la Mungu na nguvu za Roho Mtakatifu na, nitakwambia, tunaweza kuliua kila jitu hudumani. Kweli! Tunahitaji watu wanaoweza . . .

211 Mbona, Daudi alikuwa ndiye udhuru ulio duni kuliko wote kondeni, kwenda kupigana na jitu hilo. Yeye, mbona, alikuwa si kitu ila mvulana. Nayo Biblia ilisema alikuwa ni "mwekundu," maskini jamaa aliyeonekana mkondefu, labda mabega yameinama, amejizungushia kipande cha ngozi ya kondoo. Hakuwa na yoyote ya hizi digrii za kielimu wala kufunzwa vema. Hakujua lolote juu ya upanga. Hakujua lolote juu ya mafunzo haya yote ambayo Sauli . . .

212 Sauli alikuwa ndiye bora kuliko wote wangalikuwa nao, Askofu Sauli. Hakika, alikuwa tangu mabegani kwenda juu mrefu kuliko jeshi lote. Mbona, alikuwa—alikuwa ndiye aliyepaswa kwenda akapigane naye, bali aliogopa.

213 Na leo hii tunajua ya kwamba tunahitaji ufufuo. Tunajua tunahitaji ufufuo miongoni mwa watu. Haitahitaji Daktari wa Uungu. Itahitaji mtu mnyonge (Haleluya) atakayelichukua Neno la Mungu katika nguvu za kufufuka kwa Kristo na kukiua kitu hiki. Itamleta Kristo nchini katika . . . kuwaacha waone ya kwamba Yeye angali anaweza kuyafumbua macho ya vipofu, kuwaponya wagonjwa, kuwafufua wafu, na Yeye ni Mungu, Mshindi! Amina. Tunahitaji Daudi, asiyefunzwa katika shule za kitheolojia, tunahitaji mtu asiyejua kitu kuhusu jambo hilo, maskini mvulana mdogo wa plau ama kitu kama hicho, maskini jamaa mdogo mwenye mabega yaliyojikunyata, asiye na sura nzuri, atakayeshuka kuja barabarani akiwa na nguvu za Mungu.

214 Mama alikuwa yuafa, akasema, "Billy, nimekutumainia na kukuamini. Umekuwa nguvu zangu za kiroho, umeniongoza kwa Mungu."

215 Nikasema, "Mama, nilipokuwa mvulana...Usuli wetu, hakika, Waairishi, kidogo ungeegemea kwenye Ukatoliki." Ndipo nikasema, "Kanisa lilisema ya kwamba—ya kwamba wao—wao walikuwa ni kundi la watu, walikuwa na yote, kila kitu walichofanya kilikuwa ni sahihi. Nisingeweza kuamini hilo, kwa sababu Walutheri walisema, 'Sisi ni kundi la watu, tuna yote.' Wabaptisti walisema, 'Sisi ndio lile kundi, tunayo yote.' Wapo wengi sana, kuna karibu madhehebu mia tisa mbalimbali." Nikasema, "Mama, nisingeweza kuweka tumaini lolote humo, ni lipi kati ya hayo lililo sahihi?"

216 Nikaja kugundua, ninasema hili kwa unyenyekevu na utamu, bali ninaamini hakuna moja la hayo lililo sahihi. Hiyo ni kweli. Nikarudi kwenye Neno la Mungu, nikaona kile lilichofanya huko nyuma. (Halafu, Mungu, jalia sisi sote turudi kule nyuma.) Na pamoja na udhaifu, na pasipo kuungwa mkono na shirika, pasipo kuungwa mkono na madhehebu, pasipo na kuungwa mkono na mashirika ya kikasisi, bali katika urahisi na nguvu za Roho Mtakatifu zilizoshuka kwenye Pentekoste, pamoja na ujumbe ule ule ambao Petro alikuwa nao kwenye Siku ya Pentekoste, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu."

217 Hamtafungwa nira kama kundi la hawa wanatheolojia, huku ukosi wenu umepinduliwa na mna Digrii za Sanaa. Lakini, ndugu, utakuwa na kitu mkononi mwako, na mradi Roho wa Mungu ataingia kwenye hilo Neno litashinda na kuwarudisha hao kondoo wapotevu waliopotea. Amina! Tukirini udhaifu wetu! Tupilieni mbali Fundisho lenu la Uungu! Tupilieni mbali ujuaji wenu, uanachama wenu! Jivueni mbele za Mungu, tukinena kiroho, na kujiita "wasiostahili!" Ndipo Mungu anaweza kuwatumia. Usiliseme tu kutoka mdomoni mwako, lilete kutoka moyoni mwako.

218 Yakobo, Daudi, iliwabidi kujivua. Alikuwa ndiye dhaifu kuliko wote katika umati huo wote.

219 Wazieni juu ya, labda, askari elfu kumi ama laki moja kilimani. Wote wamefunzwa, kila mmoja wao akiwa na Ph.D., kila mmoja wao akiwa na mikuki, walikuwa ni askari. Kila mmoja wao alikuwa ni kopro *Nanii*, Afande *Nanii* (hata kufikia akina Afande), Jenerali *nanii*, Luteni *Nanii*. "Jenerali mkuu mwenye nyota nne Sauli, Askofu, naam, Mheshimiwa, Bwana!" Kila mmoja wao amesimama pale, watu waliofunzwa.

220 Naye adui amesimama kilimani, akasema, "Enyi kundi la waoga." Loo!

221 Na huko kambini akapanda jamaa mdogo, mwenye mabega yaliyoinama, (Ee Mungu!), jamaa aliyeonekana mwekundu,

yuna kombeo dogo mgongoni mwake, ameshika sambusa ya zabibu iliyokaushwa kwa ajili ya ndugu yake. Ndipo jitu hilo likajitokeza na kupiga kelele mara kwa mara. Kasema, "Mnataka kuniambia ya kwamba enyi hapa kundi la wasomi waliofunzwa mtasimama hapo na kumwacha Mfilisti huyo asiyetahiriwa kulitukana Neno la Mungu aliye hai?" Amina! Kasema, "Hivi mnamwogopa?"

222 Sauli akasema, "Iwapo unataka kwenda, njoo hapa. Nita—nita—nitakutuma shuleni kwa muda wa miaka ishirini sasa, na nitakupa P—Ph.D. Nitakwambia nitakalofanya, nitakupa tu digrii yangu."

223 Akasema, "Kiondoe kitu hiki." Loo, jamani! "Sitaki uhusiano wowote nacho." Yeye alitaka kumtumainia Mungu. Akasema, "Ninajua yale Mungu aliyonitendea kwa *hili*, nami niko tayari kumtumainia Mungu mbele ya kitu chochote nalo." Amina! Huo ndio ujuzi wa Mkristo.

224 Hata Sauli, wakati ilipombidi kuondolea mbali silaha zake, alivua silaha za kikasisi, alifanya kama Daudi alivyofanya. Lakini wakati Sauli alipofika mwisho wa safari yake, yeye alisema, "Nimepiga vita vizuri." Huyo alikuwa ndiye adui wa mwisho kushinda. "Nimepiga vita vilivyo vizuri, mwendo wangu nimeumaliza, Imani nimeilinda. Baada ya hayo nimewekewa taji, ambayo Bwana, Hakimu mwenye haki, atanipa siku ile." Kasema, "Si mimi tu, bali watu wote wanaopenda kuonekana Kwake."

225 Loo, mauti yalisema, "Lakini nitakupata katika dakika chache." Nalo kaburi likasema, "Nitakufinyanga huko."

226 Akasema, "Ee mauti, u wapi uchungu wako? Kaburi, u wapi ushindi wako? Ninajua nimelala hapa katika gereza hili la Kirumi, nimefungwa minyororo, vifundo vyangu na mikono, na ni—nimepata mijeledi thelathini na tisa mgongoni mwangu. Niko hapa na machozi yakiyachoma macho yangu hata siwezi kuona tena. Siwezi kuona kwa jicho langu la kawaida, bali ninaweza kuona taji ya haki imewekwa huko ng'ambo. Vifundo vyangu vimechoka. Nimeanguka sana kutokana na mikate iliyooza waliyoitupa humu ndani, na panya wamenikanyaga, na buibui na kadhalika, hata nimedhoofika." Lakini angeweza kuyakabili mauti na kusema, "U wapi uchungu wako? Kaburi, u wapi ushindi wako?" huku minyororo ikitikisika mikononi mwake. Haleluya! (Hilo ndilo tunalohitaji.) "Kaburi, u wapi ushindi wako?"

Kaburi likasema, "Nitakuozesha, Paulo."

227 Yeye akasema, "Lakini Mungu ashukuriwe, tayari nimepata ushindi kupitia Bwana wetu Yesu Kristo."

228 Wakati alipokuwa dhaifu, u—ukasisi wake, ninii yake. . .kaida zake zote zilikuwa zimemwishia. Alikuwa amenyang'anywa makaratasi yake yote ya kufanywa kasisi.

Yeye hakuwa mfuasi wa Assemblies tena, ama ninii... lolote lao. Mnaona, hakuwa mfuasi wa lolote lao tena. Alikuwa amewapinga sana hata maaskofu walikuwa... kasema, "Unataka kuniambia ya kwamba mtu anayetumikia miaka ishirini katika gereza la Kirumi huko juu anaweza kutwambia tusiwaruhusu wanawake wetu wahubiri? A-ha! Usije ukatwambia hilo," kasema, "tunajua vema zaidi. Ni nani jamaa yule kule juu, hata hivyo, anayetwambia tufanye *hili*, *lile* ama *lingine*?" Kasema, "Tunajua tunalofanya."

229 "Naam," Paulo alisema, "wapo watu wanaoinuka moja kwa moja miongoni mwenu, wataunda dhehebu hivi karibuni sana, watainuka na wataondoka kwa Imani namna hiyo, kwa kutokuwa na Roho wa Mungu." Kasema, "Tayari wametoka kwetu maana hawakuwa wetu."

230 Na, nini, je! lilitukia? Kaingia moja kwa moja katika kanisa Katoliki; kutoka Katoliki wakaingia kwenye la Lutheri; na kuendelea mpaka lile la mwisho, Assemblies of God, jambo lile lile, wakifanya jambo lile lile.

Wakati wote, jambo lile lile!

231 Lakini, loo, kwa mwanamume ama mwanamke aliye dhaifu vya kutosha, unayetambua udhaifu wako, utakayemwacha Mungu akutumie! Ninaendelea tu kuzungumza, nadhani ninazungumza kwa muda mrefu mno.

232 Sasa, ilikuwa ni kitu gani? Sasa, yeye alikuwa...Daudi alikuwa ndiye asiye na elimu kuliko wote kwenye kundi hilo. Hakuwa na mafunzo ya vita, hakujua lolote kuihusu. Kwa hiyo hakuwa na mafunzo ya yoyote ya vita hivi vilivyowekwa mbele zake, bali alitambua ya kwamba kulikuwako na Mungu. Naye akachukua kitu kilicho dhaifu kuliko vyote; wao walikuwa na mikuki, mavazi ya kujihami, nyuta, na chochote kile, naye Daudi alikuwa na kombeo dogo likiwa na jiwe ndani yake. Lakini, unaona, yeye alijua kile alichoweza kutumainia. Alikiri udhaifu wake, ila imani yake katika Mungu.

233 Akasema, "Sitaki ngao juu yangu ya kugonga chochote. Sitaki kupanda kuja huko, niseme, 'Sasa, hivi ninyi ndugu mtashirikiana nami? Mimi ni mfuasi wa Assemblies, mimi ni mfuasi wa Presbiteri, mimi ni Mmethodisti, mimi ni Mbaptisti, hivi ninyi ndugu mtashirikiana nami?' Sitaki kujua wowote wa upuuzi huo. 'Hapa, nitawaonyesha kwenye mfuko wangu, nina digrii yangu. Ndiyo kwanza nipate Digrii yangu ya Sanaa. Nimetoka kwenye Chuo Kikuu cha *Ninii*, ni—nilisomea huko. Niliipata kweli. Loo, ninaweza kuzungumza! Mimi ni *hiki, kile* ama *kinginecho*.'" Hakutaka wowote wa upuuzi huo!

234 Yote aliyotaka, yeye alisema, "Ninamtumaini Mungu na mimi hapa naenda." Jambo ndilo hilo. Nalo jitu likabwagwa chini. Hiyo ni kweli.

235 Hilo ndilo tunalohitaji leo hii, ndugu. Tunahitaji, leo, watu kama Daudi, sio ujuzi wa chuo kikuu.

236 Ilikuwa ni maskini Mikaya, maskini Mikaya, mwana wa Imla, maskini, aliyekataliwa, aliyefukuzwa kutoka madhehebu yote kwa sababu ya msimamo wake wa kweli kwa ajili ya Mungu. Lakini alitokea mtu wa Mungu wakati mmoja, huko chini, jina lake Yehoshafati, na kusema mle ndani, "Ninataka kujua Neno la kweli la Mungu."

237 Sauli akasema, "Nina mia nne wa walio bora kuliko wote uliopata kujua." Kasema, "Wote wana digrii zao, wote wamefunzwa hapa juu shuleni." Kasema, "Mbona, hao ndio wahubiri bora kuliko wote uliopata kusikia." Kasema, "Nitawaleta moja kwa moja nasi tutamtaka Bwana shauri kwa ajili yako."

238 Lakini basi alitoka akaja kule nje na kuangalia kote, Yehoshafati akasema, "Naam, ninamsikia huyu akisema *vile*, na ninamsikia yule akilisema, lakini" kasema "je! una mwingine? Hivi huna mwingine?"

239 Mungu alikuwa anataka kuupeleka ujumbe kwenye moyo huu wa kweli. Kulikuwa tu na mmoja wao aliyesimama pale, bali Mungu ana mtu kwa ajili ya huyo mmoja. Amina. Kama kuna moyo mmoja tu wa kweli, mahali fulani Mungu anaye mtu kwa ajili yake. Yehoshafati alikuwa ni mtu halisi, mfalme mcha Mungu, naye alikuwa na akili ya kutosha kujua ya kwamba jumbe zao zilikuwa ni za uongo. Alijua zilikuwa ni kinyume na Neno, amina (Loo, Ndugu Neville!), Yehoshafati alijua hilo.

240 Akasema, "Vema, ni—nimepitia taarifa yote, chati hapa kwenye seminari hii, nina kila mmoja wao hapa nje." Kasema, "Vema, angalia hapa, huyu ana . . . vema, angalia digrii alizo nazo. Mwangalie huyu hapa," anasema, "angalia—angalia digrii alizo nazo. Mwangalie Zedekia hapa, yeye ndiye kiongozi wao wote. Mbona, yeye ni askofu, yeye ni mkubwa wetu sisi sote. Hakika utaliamini neno lake!"

Yehoshafati akasema, "Naam," kasema, "Mimi—mimi—mimi . . . "

241 "Vema, angalia, angalia, hao wengine wote wanakubaliana naye. Wote wana umoja mkuu! Na huwezi kusema kuwa hao si Waebrania. Huwezi kusema hao si manabii, hii hapa digrii inayothibitisha ndivyo walivyo."

242 Yehoshafati akasema, "Naam, na—na—najua, Ahabu." Kasema, "Hilo—hilo ni sawa, ila . . . "

243 Kasema, "Unaninii . . . Utaniombaje mtu mmoja zaidi? Hiyo hapo shule yangu nzima! Hilo hapo kila dhehebu pamoja."

244 "Lakini hivi huna mmoja asiye wa kundi hilo? Hivi hakuna mmoja, mahali fulani?"

245 "Vema, angekuwa ni nini? Angekuwa mjinga asiye na elimu! Vema, ungetaka nini na jamaa kama huyo?"

246 "Lakini—lakini ninakuuliza tu, hivi huna mmoja, mahali fulani?"

247 "Loo," akasema, "naam, kuna mtu kama huyo." (Hapo, loo, Mungu ashukuriwe kwa ajili ya huyo!) "Kuna mtu kama huyo, ila" kasema "namchukia. Na hao wengine wote wanamchukia, pia." Kasema, "Tulifukuza, nao walimfukuza kwenye dhehebu lile, kila moja la hayo." Kasema, "Yeye alishuka akaja hapa kufanya mkutano, tukamfukuza kutoka mjini. Naam, bwana. Hatutakuwa na uhusiano wowote naye. Vema," kasema, "yeye ni mnyonge, naye anatoka kwenye familia maskini sana. Sarufi yake ni mbovu mno." (A-ha, kama Moody, mwajua.) "Naam, sarufi yake ni mbovu mno." Kisha kasema, "Kweli, kwa mwanatheolojia, yeye ndiye duni sana niliyepata kumsikia. Kamwe sijasikia kitu kama yeye. Loo, yeye kwa jumla huangamiza kanuni yao. Mbona, Imani yao ya Mitume inararuliwa vipande-vipande naye. Sijapata kusikia kitu kama hicho! Loo, yeye anairarua tu, nao wanamchukia nami ninamchukia, kila mtu anamchukia."

248 "Loo," Yehoshafati akasema, "mfalme asiseme hivyo, bali ningetaka kumsikia." Yeye alijua kile Elisha angesema! Alijua ni kitu gani.

249 Mungu aliwapita wahubiri wote walio wakuu, wenye nguvu, wenye elimu, na kuweka Ujumbe Wake ndani ya jamaa mdogo aliyedai kwamba hakujua kitu. Lakini alifanya nini?

250 Walimpa jaribio, na kasema, "Sasa, wewe sema jambo lile lile walilosema."

Akasema, "Nitasema yale Mungu anayoweka kinywani mwangu, hivyo tu."

251 Akasema, "Ukitaka kuwa na nguvu sasa, kumbuka wewe ni ninii tu . . . uko—kwa namna fulani umekiuka utaratibu hapa, jamani. Kumbuka, umefukuzwa kwenye dhehebu hilo. Huenda wakafikiria tena ushirika wako kama tu ukikubaliana nao katika wakati huu wa hatari jinsi hii. Sote tunajiandaa kufanya uamsho mkubwa," kasema, "ikiwa tu utakubaliana nami."

252 Kasema, "Sitasema kitu ila kile Mungu alichosema!" Kupatana, je! ungemtarajia mtu wa Mungu kupatana juu ya Neno la Mungu? La, bwana, hakumo ndani yao.

253 Kasema, "Lakini u mnyonge. Umetokana na familia maskini. Mbona, unajua nini, huenda wao . . . "

"Sijali watafanya nini."

254 "Vema, watakuchukua kutoka nchi moja hadi nyingine kwa ndege. Watafanya chochote, unaona, kama ukininii—ukininii tu . . . "

255 "La, la. Nitasema tu kile Mungu anachoweka kinywani mwangu." Mungu alikwepa kundi hilo lote, (naam, bwana, msimamo wake wa kweli ulifanya hilo) akawakwepa hao mia nne na kumpa BWANA ASEMA HIVI!

256 Basi waliamini Hilo? La, bwana! Wao walisema, "Hiyo si BWANA ASEMA HIVI, seminari yetu haifundishi mambo kama hayo. Vema, huyu hapa askofu wetu, tayari amesema neno, aliandika kile kiada. Sote tulikusanyika, tukaanzisha shule zetu. Mungu yu pamoja nasi! Mungu alipitia njia gani kutoka kwetu wakati alipoenda kwako?"

Akasema, "Utaona, siku moja." A—ha, hiyo ni kweli.

257 Yeye alikuwa nini? Alikuwa mnyonge, bali alikuwa ndiye mwenye nguvu kuliko wote miongoni mwao. Kwa nini? Kwa sababu alikuwa na Neno la Bwana. Loo, ndugu, inaleta tofauti gani juu ya . . . chochote kile mradi tu una BWANA ASEMA HIVI?

258 "Aisee, Ndugu Branham, kama utapatana juu ya Jina la Yesu kwa ajili ya ubatizo, vema, tutafanya mkutano mkubwa Chicago ama sehemu hizi namna hii." A-ha! Mnafikiri mtafanya hivyo? Sijali mnakutana wapi, yale mnayofanya, ndugu, dumu na BWANA ASEMA HIVI.

259 Ninataka baadhi yao waje waniambie ambapo Hilo ni kosa. Nionyesheni katika Neno la Mungu ambapo Hilo ni kosa. Naam. Hawatakabiliana na hilo. La, bwana. Bali ni BWANA ASEMA HIVI! Dumuni Nalo, kama kila moja la hayo litakufukuza. Sijali utakuwa dhaifu jinsi gani. "Ndipo ninakuwa na nguvu." Watakaponitupa nje, Mungu atanichukua. A—ha, naam. Mungu . . . Wakikufukuza, Mungu atakuchukua.

260 Kumbukeni, waliotupwa nje ndio Mungu huokota, watu ovyo. Ndipo anawafanya watu *wa maana* kwa ajili Yake. Huenda isijulikane katika maisha haya, bali itajulikana katika yale yajayo; unaona, hayo ndiyo.

261 Naye akampa BWANA ASEMA HIVI, kwa nini? Yeye alidumu na Neno. Alikuwa na Ujumbe wa kweli. Mungu alimpa ono. Hao wengine hawakuwa na ono. Unaona? Alikuwa na ono. Kwa nini? Kwa kuwa alidumu na Neno. Hapo ndipo tulipoona ishara na maajabu. Kwa sababu . . . Hao wengine wanajifanya kama Hilo, bali yeye alidumu na Neno. Sasa hebu na tuharakishe.

262 Eliya, ni wakati kanisa lake lilipokuwa limemkataa na kumwacha kwa ajili ya ulimwengu wa kisasa. Ninawazia Eliya alikuwa amewachambua kwelikweli juu ya makaa. Hivi hamwazii hivyo? Mnajua kile Eliya alichokuwa. Ninawazia, katika huduma yake ya mwanzoni, yeye alisimama pale na kusema, "Mbona, ninyi wanawake mnaojaribu kuwa kama Mama Taifa," kofia hizo juu yao, mwajua, "Bi Yezebeli! Ninyi wanawake wa kisasa, mkiwa kama Mama Taifa wa nchi, mkivaa

kama yeye, mkitenda kama yeye. Ninyi wahubiri!" Loo, jamani, jinsi alivyowachambua! Nao wakaendelea kupungua mpaka hapakuwapo na mtu yeyote.

263 Ilimbidi kufikia mwisho wa safari yake. Hakuna mtu angeweza kushirikiana naye tena. Hakuna moja la hayo makanisa lingeshirikiana naye. Kanisa lake lote lilimwacha, likarudi ulimwenguni (kama ilivyo sasa), hiyo ni kweli, likarudi ulimwenguni. Wachache tu ndio walikuwa wakishikilia, mmoja hapa na mmoja pale, wakija kutoka kote nchini ambako ilikubidi kwenda kumwona, na kadhalika. Alikuwa katika hali mbaya mno, alikuwa amefikia mwisho wa maarifa yake.

264 Akasema, "Bwana, nilisimama juu ya Neno Lako, nilisema Kweli. Na wote wameondoka, hakuna mtu aliyesalia hapa. Sina, hata sina mtu wa kumhubiria." Amina. "Naam, nilisimama juu ya Neno Lako, Bwana, na sasa angalia mahali nilipo sasa, hakuna hata mmoja wao atakayenipokea. Ninaingia mjini, wao wanasema, 'Huyu hapa anakuja yule maskini mwendawazimu. Naam, naam, huyu hapa maskini mwendawazimu anakuja mjini, sasa ataanza ku—kupayuka-payuka juu ya maisha haya ya kisasa na kila kitu."

265 "Msimkaribishe! Mchungaji, usishirikiane na jamaa huyo! La, bwana!'"

266 Mchungaji, "Sasa maskini yule mlokole yumo mjini tena. Unaona, yule Eliya huko nje, maskini yule mzee mwenye upara. Kamwe msimjali maskini mzee yule. Hebu mwangalie, hata havalii kama kasisi pamoja na mavazi yake ya kikasisi kama yangu (kofia yake, mwajua; na kusimama mbele, na ukosi uliopinduliwa, wajua)." Kasema, "Yeye haninii . . ." Kasema, "Yeye—yeye—yeye—yeye ni aina tofauti ya . . . Yeye—yeye ni jamaa wa kipekee."

267 Na ninawazia baadhi ya wale jamaa mashuhuri walisema, "Unajua nini? Yeye—yeye ni wazimu. A-ha, naam, yeye ni—yeye ni wazimu, akiishi huko nje nyikani, akikaa mwituni karibu wakati wake wote, akija amejizungushia kipande cha ngozi ya kondoo. Loo, jamani! Na halafu anawahukumu hao wanawake! Sijapata kuona kitu kama hicho. Msininii . . . msi—msi—msiwe na uhusiano wowote naye, hata kidogo! Msishirikiane!"

268 Vema, shirika la wahudumu lilikuwa limekusanyika pamoja, mwajua, kasema, "Msi—msiwe na uhusiano wowote . . . Mwachilieni, hatimaye ataninii . . . atafika mwisho wa akili yake. Mwacheni—mwacheni apige makelele mpaka kichwa chake kipasuke. Hivyo tu, mwacheni tu."

269 Lakini maskini Eliya, akitembea moja kwa moja mwaminifu kwa Mungu, (Jamani, jamani.) alidumu moja kwa moja na Neno. Wangefanya mkutano mdogo huko chini, naye angeangalia kwenye wasikilizaji, aseme, "Enyi Mayezebeli wote!"

270 "Loo, ujasiri wenyewe! Kamwe sitaenda kumsikiliza mtu huyo tena! La, bwana, kamwe sitamsikiliza!"

271 Hilo halikumkomesha, alidumu papo hapo vivyo hivyo. Wakati alipolipoteza kanisa lake, wakati alipopoteza ninii yake. . .madhehebu yote yalipogeuka dhidi yake, ilikuwa ni wakati huo (alipodhoofika) alisema, "Mimi ndimi tu niliyesalia, nao wanatafuta kuniua." Kasema, "Wangenipiga risasi kama wangeweza kuponyoka na hilo." A—ha. Mnaona? "Bali mimi . . . Wanayatafuta maisha yangu. Nami ndimi tu niliyesalia, Bwana, nifanye nini?"

272 Ilikuwa ni wakati huo, alipodhoofika (hata hivyo akidumu mwaminifu, akikiri udhaifu wake na kila kitu), ambapo Mungu alisema, "Njoo huku juu mlimani, nitakupa ujumbe mpya. Nitakutumia ujumbe mpya sasa. Tayari nimekwambia, 'Nenda ukayahukumu mambo haya,' sasa nitakutuma urudi na kitu cha kuthibitisha Hiyo ilikuwa ni kweli." Kasema, "Umefanya kazi nzuri, Eliya. Uliwaambia juu ya Mama Taifa, na yote hayo, na jinsi walivyofanya. Ulimhukumu Ahabu na mambo yake yote ya kisasa na makanisa yote ya kisasa, na tukawaambia hao wahubiri mahali pao. Ulikuwa mfano. Ulisimama pale pasipo na msaada wowote, dhehebu lolote, chochote nyuma yako, bali ulidumu na Neno Langu. Sasa nitakupa kitu fulani. Shuka uende huko ukamwambie yule mnafiki, 'BWANA ASEMA HIVI! Hakutakuwako hata umande utakaoanguka kutoka Mbinguni mpaka niuagize.'" Jamani! Jamani! Akampandisha juu ya mlima kumwonyesha jambo fulani!

273 Loo, ninaweza kumwona asubuhi hiyo, akija, akitembea kwenye barabara hiyo ya Samaria. Hakuonekana wa kuvutia sana, hakika, hicho kichwa chenye upara kiking'ara kwenye jua, mvi na masharafa yakining'inia usoni mwake, kipande cha ngozi ya kondoo. Biblia ilisema alikuwa mtu "mwenye nywele nyingi," amejaa nywele, ninawazia alionekana mbaya sana; maskini fimbo hiyo ndogo mkononi mwake, huku maskini hayo macho madogo yakiangalia moja kwa moja kuelekea angani, akitembea barabarani. Nanyi . . . yeye . . . Nadhani alitenda kama mtoto mwenye umri wa miaka kumi na sita wakati akiwa na yapata umri wa miaka themanini. Huyu hapa akija, akitembea barabarani, moja kwa moja hata Samaria. Ndugu, yeye alikuwa tayari ametiwa nguvu basi katika udhaifu wake, "Uweza Wangu watosha. Usijali juu ya madhehebu, Eliya. Usiyajali, Uweza Wangu tu ndio unaohitaji."

274 Ninakumbuka nikisimama karibu na hekalu kubwa wakati mmoja, na kusema, "Bwana, ningechukia wao kuja ofisini mwa—mwangu."

Akasema, "Mimi ni Sehemu yako." Unaona? "Mimi ni Sehemu yako."

275 "Ka—katika udhaifu basi ni—nina...Uweza Wangu una nguvu. Mapenzi Yangu makamilifu yanaweza kutendeka (Paulo, ama Eliya, hata uwe nani) unapoondoka njiani." Unaona? "Katika udhaifu wako, basi ninatiwa nguvu. Mimi Ndimi! Mimi Ndimi Mwenye Nguvu ambaye huingia na kujaza."

276 Ninaweza kumwona akitembea moja kwa moja kwenye hiyo barabara ya Samaria, maskini macho hayo madogo yakiangalia namna *hiyo*, jamani, kwa namna fulani ana tabasamu nusu usoni mwake. Ndugu, aliendа moja kwa moja mbele za Ahabu. Kamwe hakugugumiza maneno, kamwe hakuwa na kigugumizi. La, la! Ndani ya kifua hicho kilichokonda kulidunda moyo uliokuwa na Roho Mtakatifu akiishi mle ndani. Naam, kweli! Akaja akitembea kwenye barabara hiyo, akapanda akaja moja kwa moja mbele ya Ahabu, na kusema, "Hata umande hautaanguka mpaka nitakapouagiza."

277 Akakanyaga kwa miguu yake kisha, akageuka, huyo akarudi nyikani. Kasema, "Hiyo ilikuwa ni kazi nzuri, Eliya. Njoo huku juu, nimewaagiza kunguru wote wakakulishe sasa, na ninii... nawe ukaketi hapa juu kwa kitambo kidogo." Loo, jamani!

278 Wakati alipokuwa dhaifu, ndipo akawa na nguvu. Naam, bwana. Yeye alizifunga mbingu kwamba isinyeshe. Hapo ndipo alipokuwa na nguvu, wakati alipolipoteza kanisa lake, akapoteza kila kitu alichokuwa nacho, kila kitu kingine. Bali alidumu pamoja na Neno la Mungu, ndipo akawa na nguvu za kuzifunga mbingu.

279 Wakati Yakobo alipopoteza nguvu zake zote, ndipo Mungu alipompa nguvu za kuwa mtawala. Unaona?

280 Wakati Paulo alipopoteza elimu yake na theolojia yake yote, Mungu alimfanya mmishenari kwa Mataifa.

281 Wakati Musa alipopoteza uwezo wake wote na akawa dhaifu, Mungu alimpa nguvu na kumtuma Misri kwa nguvu za Roho, akiwa na umri wa miaka themanini; masharafa yakining'inia chini, mkewe juu ya nyumbu na mtoto ameketi kwenye paja lake, na fimbo mkononi mwake, akashuka akaenda akaishinda Misri. Naam. Unaona? Sio akiwa na jeshi nyuma yake, kama vile alivyotaka kwenda, bali katika nguvu za Roho. Amina!

Unapokuwa dhaifu ndipo una nguvu.

282 Akitembea tu kwenye barabara hiyo, hakugugumiza, hakujikwaa, hakufanya chochote, akaenda moja kwa moja mbele ya Ahabu, na kusema, "Ninalo Neno la Bwana."

Akasema, "Wewe ndiwe unayetaabisha Israeli."

283 Akasema, "Wewe ndiwe mtaabishaji wa Israeli." Naam, bwana. Loo, ndugu! Naam, bwana. "Walete huku hao makuhani wa kielimu ulio nao huku juu, na hebu tuone ni nani aliye Mungu." Haya basi. "Panda juu ya Mlima Karmeli, hebu Mungu aliyejibu huko Pentekoste ajibu tena. Hebu tuone kama Mungu

angali ni Mungu yeye yule, kama Yesu ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Akashuka kutoka mlimani, alikuwa na Ujumbe. Naam. Alikuwa dhaifu sana hapo kabla, hata hivyo, akapoteza kila kitu kabla ya kufanya hivyo. Ilibidi awe dhaifu kabla hajapata kuwa na nguvu.

284 Ni urahisi wa Injili ndio unaowayumbisha watu. Wanajaribu kuifanya kitu fulani kikuu cha kielimu ama kingine, wakati ni urahisi. Lakini Mungu huchukua chombo kile kile cha unyenyekevu na udhaifu na urahisi, apate kutenda kazi Zake kwake. Hicho ni chombo tu mkononi mwa Mungu.

285 Yohana Mbatizaji, Ujumbe wake, yule mtangulizi wa Kristo, rahisi sana hata lilipitia juu ya vichwa vya watu hao. Sikilizeni tu kwa dakika moja. (Natumaini siwaweki sana, ninyi mnaosimama kuzizunguka kuta, mnaona.) Angalieni! Yohana, wakati. . .Manabii wote walitoa ushuhuda juu ya kuja kwa Masihi. Mmoja wao alisema kwamba "Milima itaruka kama wana kondoo wadogo." Wengine walisema, "Majani yatapiga makofi." Mmoja alisema, "Mahali pote palipo chini patainuliwa, na palipoinuka patashushwa." Loo, jamani! Ni siku ya jinsi gani!

286 Hivi uliwazia Shule ya Manabii na dhana za kielimu juu ya hilo? Loo, jamani, waliweka kila kitu kimtindo sana! Lakini wakati lilipotukia, kutoka nyikani akaja maskini mhubiri ambaye hakwenda shuleni hata siku moja maishani mwake, labda sarufi yake ilikuwa mbovu sana. Baba yake alikuwa ni kuhani, bali Mungu alimwondoa katika huo. (Tulikuwa nalo katika somo la Jumapili iliyopita.) Asingemruhusu kujichanganyisha na madhehebu hayo, ndipo akampeleka nyikani apate kumfunza Mwenyewe. Hao ndio—hao ndio aina ile watakaodumu na Neno la Mungu.

287 Akatoka nyikani, akiwa na karibu umri wa miaka thelathini; ninawazia ndevu nyeusi zikining'inia usoni mwake, za kipilipili; amejizungushia maskini kipande kikubwa cha ngozi ya kondoo; amesimama kwenye matope, kufikia magotini mwake; kasema, "Mimi ndimi niliyenenwa habari zake na nabii Isaya." Ndipo baadhi ya hayo madhehebu yakatokea; yeye akasema, "Msifikirie kusema mioyoni mwenu 'Tuna *hiki* na *kile*,' Mungu anaweza kutoka kwenye mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto!" Loo, jamani! Kwa nini? Yeye alikuwa na BWANA ASEMA HIVI! Alikuwa na Ujumbe. Mungu alitabiri alikuwa anakuja. Na sababu yake. . .Yeye alikuja katika urahisi sana, hata Hilo likapitia juu ya vichwa vyao.

288 Yesu alipokuja, Yeye alisema, "Mlitoka kwenda kuona nini, msemaji wa kielimu anayeweza kubadilishwa kutoka Methodisti aingie Baptisti, na kutoka Baptisti hadi Presbiteri, kutoka Presbiteri hata Pentekoste, na Pentekoste hadi kwenye kitu kingine? Mlienda kuona unyasi unaotikiswa na upepo wowote?

Sio Yohana!" Kasema, "Je! mlitoka basi kwenda kumwona mtu aliyevaa mavazi mororo?" Akasema, "Hao wako kwenye nyumba za mfalme, mhudumu wa namna hiyo." Akasema, "Basi mlitoka kwenda kuona nini, nabii?" Akasema, "Zaidi ya nabii!"

289 Yohana alikuwa ni zaidi ya nabii. Na, angalieni, alikuja mnyenyekevu kuliko hao wote. Bali alikuwa ni zaidi ya nabii. Mnajua kile Yohana alichokuwa? Alikuwa ni mjumbe wa agano. Hakika, alikuwa. Alienda zaidi ya nabii. *Nabii* ni mwonaji anayeona mambo. Yohana aliyaona, pia, lakini alikuwa ni zaidi ya hapo. Alikuwa ni mjumbe wa agano. Alisema, "Naam, huyu ndiye aliyesemwa 'Nitamtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wako.'" Hivyo ndivyo alivyokuwa, alikuwa ni mjumbe wa agano. Hakika. Katika njia yake rahisi ya kuja, liliwapofusha tu wenye elimu.

290 Sasa hatuna budi kufunga upesi sana, kama dakika chache zaidi, nina mambo machache hapa ninayotaka kusema, Maandiko machache na muhtasari.

291 Vipi kuhusu yule mjane mwenye konzi la unga? Alikuwa ameufikia udhaifu wake, labda alijinyima chakula hata kufa. Hakuwa na unga. Asingeweza kwenda mahali pengine popote na kuomba unga, hakuna mtu mwingine aliyekuwa nao. Lakini alifikia mahali, mwaminio hodari, mumewe alikuwa ni mtu hodari wa Mungu. Naye alikuwa mjane, akiwa na mtoto. Naye alikuwa na konzi moja tu la unga, bali ulitosha, huo tu ndio aliohitaji; ulipowekwa wakfu mikononi mwa Mungu, aliishi kwa huo kwa muda wa miaka mitatu na miezi sita, kwa konzi la unga. Akawa dhaifu.

292 Alitoka asubuhi hiyo kwenda kuokota kuni mbili, na kuzivunja na kuziweka pamoja. Unaona, hizo kuni mbili ni Msalaba. Unaona? Kuvunja... Akasema, "Ninaenda kuokota kuni mbili." Kamwe hakusema "Nitaokota nijaze mikono," sasa, kuni mbili tu. Hizo tu. Unaona mfano wake?

293 Na, naam, maskini njia ya kale... Njia ya kuuwasha moto sasa, ni kuchukua magogo na kuyakingamiza, ukayachome katikati hasa. Ninapoenda kupiga kambi, mimi... milimani wakati wa usiku, nisije nikaganda, mimi hulilaza gogo *hivi*, na gogo *hivi*, na usiku ninaendelea tu kuisukuma miisho yake, nayo inaungua moja kwa moja namna hiyo unapoendelea, unaona, moja kwa moja kupitia msalaba.

294 "Nina kuni mbili. Nitaoka mkate, nitaukanda unga huu, konzi hili moja dogo la unga, na kuoka mkate wangu na mtoto wangu. Tule kisha tufe." Alikuwa kweli katika udhaifu, sivyo? Akasema... Naye akageuka na kuanza kurudi nyuma. Loo, asubuhi hiyo yenye joto! Loo, ilikuwa imekuwa muda mrefu wakati huo bila chochote. Kila kitu... Hakuna maji, na watu wakipiga mayowe, watu wakifa, kila mahali; hakuna mahali pa kukopa, hakuna la kufanya. Alikuwa amefika mwisho. Alikuwa

katika udhaifu wake. Alisema, "Nitauoka kwa ajili yangu na mwanangu, na halafu tutakula na kufa." Kwa hiyo akageuka na akasema . . .

295 "Hebu kidogo!" Akaangalia nyuma. Na maskini ule uso wenye nywele za kipilipili ukitokeza langoni huko chini, kasema, "Nenda kanipikie mkate mdogo kwanza, ukanileteee." Loo! "Nichotee maji kidogo mkononi mwako, na kipande cha mkate, kwa kuwa, BWANA ASEMA HIVI!" Loo, jamani, hilo lilitosha. Loo, jamani! Ule mdogo sana aliokuwa nao, mnaona, aliuweka wakfu kwa Mungu. Huo ulitosha kumlisha wakati uliosalia. Naam. Mnaona, wakati alipokuwa dhaifu basi alikuwa na nguvu.

296 Mmoja alikuwa na chupa tu iliyokuwa na mafuta kidogo ndani yake. Naye hakuwa na kitu, wanawe wawili walikuwa wauzwe kama watumwa. Hakuwa na lingine la kufanya na chupa hii ndogo ya mafuta. Haikuwa chochote, alikuwa amefikia mwisho wake.

Eliya akamwambia, kasema, "Una nini nyumbani mwako?"

Kasema, "Mafuta kidogo tu katika chupa."

Kasema, "Nenda kwa majirani wako, ukaazime nyingi."

297 Hapo, angalieni, kujiandaa hata kabla halijatukia. Hmm? Jiandae! Daudi alisikia hiyo sauti kwenye vichaka vya miforsadi. Elisha aliona wingu ukubwa wa mkono, kasema, "Ninasikia sauti ya mvua tele." Laiti Mungu angaliweza kupata vyombo vitupu! Hiyo ni kweli.

Akasema, "Jaza nyumba ijae hizo." Amina!

298 Mnaona kile Mungu anachohitaji? Mungu lazima apate vyombo vitupu. Sikilizeni! Tumekuwa na mafundisho mengi sana, upuuzi mwingi sana wa kikanisa, mpaka tumefikia mwisho wa pipa. Kuna jambo moja tu lililosalia, mgeukieni Mungu na Neno Lake. Na endapo mtafanya hivyo, tafuteni vyombo vitupu. Ondoleeni mbali Methodisti yote kutoka kwavyo, Pentekoste yote kutoka kwavyo, na Baptisti yote kutoka kwavyo, na hebu wawe tu ni vyombo, kisha mviweke nyumbani. Halafu mchukue yaliyo kwenye Chombo hiki na muanze kumimina, amina, muanze tu kumimina.

299 Alikuwa na ya kutosha kujikimu mwenyewe pamoja na watoto wake, na chochote kile, na kulipia madeni yote. Kwa nini? Kwa nini? Kile kidogo tu alichokuwa nacho, alikiweka wakfu kwa Mungu, na kufuatana na neno la nabii huyu, alifaulu.

300 Mungu, tutumie nabii atakayelichukua Neno la Mungu, ambaye hatachukua kitu *fulani kingine*, ila tu kuchukua vyombo vitupu. Kama Mungu anaweza tu kupata vyombo vitupu, na kisha alichukue Neno la Mungu na kulimimina ndani ya mtu huyo.

301 Sio wengine waseme, "Loo, nilitetemeka wakati nilipompokea. Nilinena kwa lugha nilipompokea. Nilicheza katika Roho." Sahau hilo, unaona, sahau hilo!

302 Kaa tu hapo mpaka atakapokuja, hivyo tu, mpaka chombo kitakapojaa. Jambo ndilo hilo. Hivyo ndivyo unavyofanya. Naam, bwana, urahisi Wake! "Vyombo vilijaa," jinsi tungaliweza kudumu juu ya hilo!

303 Ilikuwa ni wanafunzi, wakiwa wote wamevurugika siku moja, Yesu aliwaambia, kasema, "Wapo watu elfu tano hapa," kisha kasema, "wanazimia, wanakufa kwa njaa." Loo, ningeweza kudumu kwenye hilo saa nyingine nzima. "Elfu tano, wakifa kwa njaa," kuna bilioni mia moja wanaokufa kwa njaa!

Kasema, "Waageni."

Kasema, "Hakuna haja ya kufanya hivyo." Kasema, "Ninyi walisheni."

304 Loo, jamani! Ninaweza kuwazia wakikusanya kila kitu wangaliweza kupata, nanyi mwajua walipokusanya yote (kila kitu). . .Samahani kwa tamshi hilo, "kukusanya." Lakini walichukua kila kitu, wakasema, "Sasa, hapa, tumepitia kwenye kambi yote. Hatuna hata hela moja ya fedha, kwa hiyo hatuwezi kufanya uamsho." Unaona? "Kwa hiyo tuna kila kitu hapa, bali kitu pekee tunachoweza kupata ni mikate mitano midogo na samaki wawili kutoka kwa mbilikimo mdogo" kama Daudi, aliyetoka huko nyikani. "Hiyo tu ndiyo tuliyo nayo. Hiyo tu ndiyo tunayoweza kupata. Tumechanganyikiwa kabisa. Hatuwezi kufanya lolote lingine, Yohana." Petro akasema, "Hivyo tu ndivyo tunavyoweza kufanya. Hivyo tu ndivyo tunavyoweza kufanya. Tumechanganyikiwa kabisa. Hicho ndicho kitu pekee tulicho nacho kuhusu chakula."

305 Vema, ninaweza tu kuchukua Andiko moja dogo, Matendo 2:38, na hilo tu ndilo tunalohitaji, kutii Hilo tu. Haikubidi kujifunza seminari, yote kuhusu *hiki, kile, kinginecho*, chukua tu Hilo. Naam, chukua—chukua tu Hilo, hilo tu ndilo unalohitaji, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtajazwa na hayo Mafuta." Unaona? Jiweke tu mtupu, uwe tayari kwa ajili ya Hayo, hayo ndiyo tu unayohitaji. Weka tu tone ndani yake, angalia likijaa.

306 Unajua, hapakuwapo na ya kutosha kwenye pipa hilo kumimina angalau tone moja kwa kila moja. Labda alichukua kidole chake, namna *hii*, akalimiminia katika kila moja namna hiyo; akaangalia nyuma na lilikuwa limejaa. Akayamimina tu, unaona, hilo tu ndilo alilohitaji, maana yalikuwa ni mafuta yaliyobarikiwa.

307 Usichukue ujuzi fulani wa seminari. Chukua Neno la Mungu na ulitie mle ndani, uone jinsi litakavyojaza.

308 Akasema, “Vema, inatupasa kufanya tone la aina gani? Labda tunaweza kuchukua kitu kutoka kwenye Zaburi.”

309 Ninyi chukueni nilichowaambia, “Tubuni, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi, nanyi mtajazwa kutoka kwa Tone hilo.” Litoneshe tu hilo humo ndani, nawe utajazwa kwa Tone hilo. Hilo ndilo Tone ambalo Petro alitumia kwenye Siku ya Pentekoste. Hilo ndilo Tone ambalo Paulo alitumia. Hilo ndilo Tone ambalo wanafunzi wote walitumia. Hayo mengine yataongezewa, wewe chukua tu Tone hilo na ulifuatilie, na hayo mengine yatakuwa ni sawa.

310 Kuwa dhaifu! Kuwa tupu! Toa yote, na tangu hapo na kuendelea litaendelea kudondoka, na Mungu atadondosha yaliyobaki. Wewe fanya tu hivyo. Wewe piga magoti na upokee hiyo kwa moyo wako wote. Dondosha moyoni mwako sasa hivi na useme, “Mungu, ninaamini Hilo, kwa moyo wangu wote!” Mungu atayashughulikia matone hayo mengine, litajaa, “Utaja-. . . utajazwa tena na Roho Mtakatifu.”

311 Sasa walikuwa na mikate mitano midogo na samaki wawili. Kwa hiyo walikuwa wanaenda kufanya nini? Kwa hiyo walikuja na kusema, “Hii tu ndiyo tunayoweza kukusanya. Hatujui la kufanya. Hatuwezi kupata kipande kingine cha mkate mahali popote, hakuna mtu. Na maskini mvulana huyu, labda akionyesha . . . akiwa mtoro, alienda shuleni asubuhi ya leo, akaepa shule akaenda kuvua samaki hapa chini. Nasi tukamchukua, kule kwenye kijito, akaja kusikiliza. Na, pale, yeye ana mitano.” Mungu ashukuriwe kwa ajili ya mvulana huyo mdogo! Naam, bwana. Kasema, “Sisi . . . kitu pekee tulicho nacho kuhusu maisha ni kipande hiki kidogo hapa.” Kasema . . .

312 Yesu akasema, “Hiyo yatosha. Ilete hapa.” Mnaona? “Ilete hapa, hebu niichukue. Hebu nichukue tone hilo dogo, nitashughulikia mengine yote. Sasa, ninyi endeleeni tu kusambaza wakati nikiwakabidhi kutoka kwenye tone hili.”

313 Na kila mmoja wenu na achukue hilo tone la Matendo 2:38 asubuhi ya leo, moyoni mwako, na uchukue tu kutoka hapo na umwone Yeye akianza kuwavunjia Mkate wa Uzima. Ninyi tubuni, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, na ndipo muone kama Roho Mtakatifu hatadondosha ndani, aendelee kumiminia *hili* na kumiminia *lile*, kumiminia *hapa* na kumiminia *pale*, na kumiminia *pale*, na kutakuwako na kujazwa na Roho Mtakatifu! Kweli!

314 Haikubidi kwenda kwenye seminari. Haikubidi kuwa mwerevu. Jambo pekee likupasalo kufanya ni kutambua hujui kitu. Acha Mungu akushike, Yeye atayashughulikia hayo mengine.

315 Vema, ndipo Sauti ikasema, “Walete hapa.” Hilo ndilo Mungu analotaka asubuhi ya leo, kumletea lundo la vyombo vitupu. Yeye atayashughulikia hayo mengine. Naam, bwana.

316 Kipofu Bartimayo akiketi langoni, ameparuza, ni baridi, loo, wakati wake ulio dhaifu kuliko zote, wakati aliposikia Sauti, kasema, "Mleteni hapa." Hiyo ni kweli, wakati mwingine ni wakati wako ulio dhaifu kuliko zote.

317 Kulikuwako na Mariamu kaburini, amevunjika moyo, Mtoto wake mchanga, Mvulana wake alikuwa ameuawa, kila kitu, matumaini yote yalikuwa yamekwisha. Naye akaenda kumtia dawa asioze, na hata mwili Wake haukuwapo. Ndipo akasikia Sauti ikisema, "Mbona unalia, ewe mwanamke?"

318 Akasema, "Wamemchukua Bwana wangu. Na mimi . . ." Maskini jamaa mdogo, Mtoto wake ndiye aliyekuwa ameaibishwa; wakamvua nguo akawa uchi wa mnyama na kumsulibisha huko juu Msalabani, kisha wakamsulibisha na kumpigilia misumari pale juu, akiisha kudai kuwa ndiye Masihi, akisha kujua ya kwamba Roho Mtakatifu alimtia uvuli na akamzaa Mtoto huyu. Alikuwa ni Mtoto wa Mungu. Alikuwa ameziona kazi Zake, na kila kitu, na akaona moja kwa moja katika wakati ulio dhaifu kuliko zote . . .

319 Na pale Yesu alikuwa ameyapinga maovu, akapinga hayo madhehebu, akawakemea hao Mafarisayo; kisha akawa dhaifu na kujitolea Mwenyewe hata kufa, na akafa kama mwenye dhambi Msalabani, akizichukua dhambi zetu. Zaburi yenyewe, wale manabii wenyewe waliowaamini, walikuwa wameyanukuu (mamia ya miaka hapo kabla) Maneno yale yale aliyoyasema pale Kalvari, nao wakashindwa kuona jambo hilo. Ninii yao kuu ya kikani-. . .

320 "Mungu wangu," kasema Daudi, "Mungu wangu, mbona umeniacha?" Zaburi 22, "Mifupa yangu yote, inanikodolea macho, hakuna hata mmoja umevunjwa. Wanatikisa kichwa chao na kusema, 'Aliwatumainia wengine . . . A—aliwaokoa wengine, hawezi kujiokoa Mwenyewe.'" Na mambo yote ambayo manabii walikuwa wamesema, yalikuwa papo hapo! Naye Yesu, akifa, akilishikilia Neno hilo, alijitolea Mwenyewe. Mungu, Imanueli, alidhoofika sana hata akajitiisha hata kufa, na akaenda kaburini, na nafsi Yake kuzimuni. Udhaifu! Lakini kutokana na huko kujisalimisha kukamilifu . . . alitokea kwenye ile asubuhi ya Pasaka, akipenya kutoka pande za chini kabisa.

321 Alikuwa wa Juu kuliko wote, kisha akawa wa chini kuliko wote. Aliwajia watu wa chini kuliko wote, akaenda kwenye mji ulio wa chini kuliko yote. Na mtu aliyekuwa mdogo kuliko wote mjini ilimbidi kumwangalilia chini. Akatoka hapo akaingia mautini, na kutoka mautini akaingia kaburini, na kutoka kaburini akaingia kuzimuni; ya chini kuliko yote iliyoweza kupatikana, kwenye kuzimu ya chini kabisa ingaliweza kuwaziwa, Yeye aliingia humo.

322 Lakini basi, kutoka hapo, Mungu alianza kumwinua juu. Kupitia Paradiso, kutoka huko akaenda—akaenda kaburini, na

kutoka kaburini akaingia Utukufuni, na Juu sana hata inambidi kuangalia chini apate kuona Mbingu. Akaviinua viti vyake vya enzi Mbinguni!

323 Maskini mama huyo aliyevunjika moyo, pasipo kujua jambo hili, amesimama pale, "Wamemchukua Bwana wangu, nami sijui ni wapi." Alikuwa. . .majira dhaifu sana aliyopata kuwa nayo. Bwana wa—wake alikuwa ametoweka. Walikuwa wamemsulibisha, hata hivyo akawaacha hawa. . .wamsulibishe katika aibu ya kumtundika pale juu akiwa uchi mbele za watu hao; kisha wakamchoma kwa mkuki ubavuni, na kutokwa na damu, na kumsikia Yeye akilia Msalabani, na kuiona nchi ikitetemeka, na mbingu zote zilitambua alikuwa amekufa. Wakamshusha chini, amekauka na ni baridi, wakamlaza kaburini. Akawazia, "Heshima ya mwisho ninayoweza kumpa Mtoto wangu mpendwa ni kuja na kumtia dawa asioze, na sasa wamemchukua." Naye alikuwa amesimama pale akilia, maskini mama huyo amesimama pale akilia, akilia kwa kwikwi. Loo, wakati dhaifu sana!

"Mbona unalia, ewe mwanamke?" ilikuwa ni Sauti nyuma yake.

324 Alidhani ilikuwa ni mlinzi kwenye makaburi, kasema, "Loo, wamemchukua. . ." Hata asingeweza kugeuka, alikuwa dhaifu sana. Akasema, "Nimekuwa macho siku hizi zote tatu usiku na mchana. Nilisimama na kuangalia kule kusulibishwa, nilimwangalia Mpenzi wangu mwenyewe niliyejua ya kwamba alikuwa ni Mwana wa Mungu. Ninajua alikuwa! Na hata hivyo wao. . ." (Akiangalia upande huo mwingine, na Yeye nyuma.) "Nao wakamchukua na kumsulibisha. Nilimwona akiwafufua wafu kutoka kaburini. Nilimwona akifanya miujiza baada ya miujiza. Nami ninajua Roho Mtakatifu. . .Mungu anaujua moyo wangu, sikuwa na hatia ya chochote, Naye Roho Mtakatifu akanipa Mtoto huyo mchanga bila ya kumjua mwanamume. Jinsi ninavyojua ya kwamba ilikuwa ni kweli! Nami nilimwona akiaibishwa na. . .akavuliwa nguo Zake, na kusulibishwa huko juu na kumvua nguo. Alikufa kifo kibaya kuliko vyote. Ninampenda, sijali yale aliyofanyiwa. Ningali ninataka kumzika, ninataka—ninataka kumpa mazishi yanayofaa, nao wamemchukua. Nimekuwa siku baada ya siku, moyo wangu umevunjika. Ninasimama tu katika hali hii. Sijui yale wamemtendea Bwana wangu."

325 Yeye akasema, "Mariamu." Ndipo akawa na nguvu. Amina! "Nenda ukawaambie wanafunzi Wangu nitakutana nao Galilaya." Loo, jamani!

326 Katika udhaifu basi tunatiwa nguvu. Unapokuwa dhaifu, hapo ndipo unapokuwa na nguvu.

327 Petro, baada ya yeye kuwa huko nje akivua samaki, alikuwa. . .kazi yake ilikuwa ni kuvua samaki. Kwa namna

fulani ninaipenda kazi yake. Na kwa hiyo, alikuwa huko nje akivua samaki, amevunjika moyo kabisa, akijua ya kwamba alikuwa amemkana Kristo. Loo, jamani! Alimsikia nabii huyo akisimama pale na kumwambia, "Petro, unasema kwamba unanipenda?"

328 Akasema, "Ee Bwana, Wewe wajua ninakupenda." Akasema, "Ninakupenda. Niko tayari kufa kwa ajili Yako."

329 Akasema, "Petro, unafikiri unamaanisha hilo, bali utanikana Mimi mara tatu kabla . . . Utanikana kabla ya jogoo kuwika mara ya tatu. Unaona, utanikana mara tatu kabla ya jogoo kuwika."

330 Na halafu akiona hilo likitimia, wakati aliposimama pale na kusema "Simjui. La, sijui lolote kuhusu wale Wapentekoste pale."

331 Sio wakati wa kuacha kuhubiri, ni saa yangu tu inaduwaa. [Kengele ya saa ya Ndugu Branham ililia—Mh.] Mnaona? Kasema kwamba . . . Na—na—najua ni—ninapaswa kumalizia sasa, bali si—siwezi kumalizia kwenye wakati uu huu, mnaona, kwa hiyo sina budi kumalizia haya hapa katika dakika moja tu.

332 Kasema, "Na—na—na—najua nilimkana. Nilimkana mbele ya Pilato. Nilimkana hadharani hapo maskini yule mwanamke alipojongea karibu nami, akisema, 'Hivi wewe si ni mmoja wao?' 'La!' Na hata nikalaani!" Loo, alikuwa katika hali mbaya sana. Kasema, "Mimi—mimi—mimi . . . " Akakana . . . Alikuwa amemkana. Naye alikuwa amemwona Yesu amesimama na kuangalia huko, hapo ndipo akawika jogoo, akamwangalia Petro. Akatoka. Loo, akajijutia, kasema, "Mbona niishi tena?"

333 Halafu basi, mbali na hayo, akasema, "Nafikiri nitarudi na niende nikavue samaki tena. Siwezi kuhubiri tena, kwa hiyo nitarudi tu na nianze kuvua samaki." Alikuwa ametupa ndani nyavu zake na kuzitupa usiku kucha, hakupata samaki wowote. Naye alikuwa katika hali ya udhaifu, hakuwa na kitu, akajijutia, akafikia mwisho wa vipaji vyake.

334 Vema, alidhani yeye alikuwa ni mtu mashuhuri, akayakata masikio ya mwana wa kuhani mkuu namna hiyo. Vema, alidhani alikuwa ni jamaa mashuhuri, mwajua, alikuwa amejifunza jambo fulani. Bali hakujua kitu! Ilimbidi kusahau yote kuhusu jambo hilo.

335 Naye huyo hapo huko nje, kasema, "Vema, ninajua jambo moja, mimi ni mvua samaki. Ningali ninaweza kupata riziki, kuvua samaki." Alitupa usiku kucha wala hakupata kitu. Loo, ni kuvunjika moyo jinsi gani! Kila alipovuta, wavu mtupu. Naye akavunjika moyo kabisa! Alikuwa katika kilele cha udhaifu, kasema, "Hata najisikia kama kuruka kutoka kwenye mtumbwi huu. Mimi sina thamani yoyote, kwa vyovyote vile."

Akasema, "Mna samaki wowote, wanangu?"

336 Akaangalia nje ufukoni, na huyo hapo Mtu amesimama. Akasema, "La, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha tusipate kitu. Nilidhani nilikuwa mvua samaki."

"Huyo ni wewe, Simoni?"

337 "Naam. Vema, nimefanya kazi ya kuchosha usiku kucha nisipate kitu. Loo, ni—ni . . . Hatuna samaki wowote hapa."

Akasema, "Vema, litupe jarife lako upande huo mwingine."

338 "Tumefanya . . . Kitu gani?" Basi aka- . . . Kasema, "Ati upande huo mwingine? Tumekuwa tukifanya hivyo!"

"Litupeni upande mwingine."

339 Akatupa majarife yake, kisha akavuta. Akasema . . . Ndipo akawa na nguvu. Loo, jamani! Akanyakua maskini vazi lake la mvuvi akajizungushia, kasema, "Ndugu, Huyo Ndiye!" Naye akawatangulia hao ufukoni kabla hawajafika, wakipiga makasia hiyo mitumbwi upesi tu walivyoweza, akawashinda kuogelea, akiwa amevaa vazi la mvua samaki, akafika ufukoni. Kwa nini? Wakati alipokuwa na nguvu. Alipokuwa na nguvu asingeweza kufanya lolote, bali alipodhoofika basi akawa na nguvu. Naam, bwana.

340 Loo, mkakati wa Mungu ni kuchukua vyombo vitupu vya kibinadamu na kuutikisa ulimwengu kwavyo. (Sasa, kidogo tu halafu tutaondoka.) Kama vile kwenye Pentekoste, huko Pentekoste, Yeye alifanya nini? Iliwachukua siku kumi kuwa tupu kabisa. Bali wote walikuwa wemesimama pale huku vyombo vyao vimepinduliwa juu, Naye Mungu akajitwaa Mwenyewe na kuwajaza. Hivyo tu! Waliutikisa ulimwengu; akajimwaga ndani yao.

341 Hayo ndiyo mahitaji ya siku hizi. Hicho ndicho tunachohitaji leo hii, ni vyombo vitupu, naam, bwana, kusudi Mungu apate kuvijaza. Wala huwezi kuvichukua . . . Sina budi kuruka mengi hapa. Mungu hawezi kuvitumia mradi vimejazwa tayari. Kama umejaa mafunzo ya kithiolojia, Mungu hawezi kukutumia. Mungu hana budi kupata vyombo vilivyo tupu kusudi *Yeye* aweze kuvijaza.

342 Sasa, Eliya hakusema, "Nenda ukachukue vyombo kadhaa kisha uazime mafuta mengi sana, nasi tutaona kama hatuwezi kupata bei nzuri ya kuyauzia, nawe upate kidogo ya ziada na unaweza kumlipa jirani namna hiyo." Alisema, "Teka tu vyombo *vitupu*. Hivyo tu ndivyo unavyohitaji."

343 Hivyo ndivyo ilivyokuwa huko Pentekoste, walikuwa na vyombo vitupu kusudi Mungu aweze kuwajaza. Ndugu, siku hii inahitaji hivyo. Siku hii; hapana budi kuwa na hivyo. Tutakuwa na hivyo ama tuangamie. Nitafunga sasa, sikilizeni. Hatuna budi kuwa na hivyo ama tuangamie. Naam, bwana.

344 Mitambo mikubwa ya kikanisa tuliyo nayo, mitambo mikubwa ya kanisa imejaa kaboni, imenoki kiroho. (Ndugu

Collins yuko mahali fulani hapa, na Ndugu Hickerson.) Nafikiri hendeli ni mbaya. Kitu fulani kimeharibika. Wanatumia petroli mbaya, imejaa kaboni. Walitumia ujuzi wa seminari badala ya Roho Mtakatifu.

345 Miamsho yetu mikuu ya nchini, watu wetu mashuhuri, miamsho yetu ya uponyaji, yote imeshindwa. Tunajua imeshindwa. Hebu mwangalieni mwinjilisti wetu mkuu, Billy Graham, amevuka nchi huku na huku, huku na huku, huku na huku. Imeleta faida gani? Oral Roberts, miamsho ya uponyaji kila mahali, na inazidi kuwa mbaya wakati wote.

346 Kwa sababu ni yote Baptisti, Presbiteri, Assemblies of God, madhehebu haya mengine mbalimbali, wanayakusanya yote pamoja, ni kitu gani? Mtambo mkubwa mno wa kikanisa, naye Mungu amewajazia yote kaboni. Sasa linatitima tu, "titima," pump, pump, pump, "titima," pump, pump, pump, kidogo hapa na pale. Limekwisha! Limeisha! Petroli imeisha, mliitia maji. Kila kitu kimekwisha (naam, bwana), tairi zilizokwisha pumzi pande zote mbili. Tuko katika hali mbaya sana. Ule mtambo wa kikanisa umekoma.

347 Na, ndugu, kifuniko cha kuzimu kimeondolewa. Hiyo ni kweli. Na mitiririko ya nguvu za pepo inamwagika kutoka kila mahali. Imeyashinda mataifa. Imezishinda siasa mpaka zimeoza kabisa. Imeyashinda makanisa hata hawajui kitu ila madhehebu.

Unasema, "Hivi wewe ni Mkristo?"

"Mimi ni Mmethodisti."

"Wewe ni Mkristo?"

"Mimi—mimi ni Mpentekoste."

348 Hilo halimaanishi zaidi ya kuwa nguruwe, kama nilivyosema hivi majuzi, ama nguruwe mwitu, ama farasi, ama chochote kile. Hilo halina uhusiano wowote Nalo. Wewe ni Mkristo wakati unapozaliwa mara ya pili na kujazwa na Roho Mtakatifu, si kabla ya hapo, na umejitolea kabisa kwa Roho. Kama hujajitolea kwa Roho, basi hujazaliwa mara ya pili wala huna Roho Mtakatifu. Huenda ukanena kwa lugha na kutetemeka, na kuruka na kukimbia, na kufanya kila namna ya . . .

349 Paulo alisema, "Ninaweza kuihamisha milima kwa imani, ninaweza kuwaponya wagonjwa, ninaweza kuwa na maarifa ya Biblia, ninaweza kwenda kwenye seminari na kujifunza upuuzi huu wote, kila kitu," kasema, "bado si kitu mimi!" Haleluya!

350 Loo, jamani, nena kuhusu kifuniko cha birika kimeondolewa! Pepo wakizunguka, nguvu za ibilisi, chini ya jina la Ukristo, "Wakifundisha Mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu," mafundisho ya seminari za kitheolojia, wakiachana na Biblia.

351 Haleluya! Ni nani awezaye kuninii, ni nani aliye na nguvu za kutosha, ni nani aliye na hekima za kutosha? Ni nani aliye na nguvu za kutosha kutiisha jeshi hili linalowavua wanawake wetu nguo, katika jina la wahubiri, Methodisti, Baptisti, na hata Wapentekoste? Huku wakipaka nyuso zao rangi kama Yezebeli, na kukata nywele zao, na kuvaa suruali ndefu kama tu wanaume. Wahubiri wetu, hawana ya kutosha kusimama na kuwaambia kuhusu hilo. Kupagawa na pepo! Yule jeshi ndiye aliyezirarua nguo zake akazitoa. Ni nani huyu pepo anayenguruma?

352 Ni nani mwenye nguvu za kutosha? Ni dhe—dhehebu la aina gani linaloweza kumshinda wakati akitembea huku na huku kupitia kwenye mawe haya ya makaburi ya kimadhehebu, akilia, "Siku za miujiza zimekwisha, wala hatuhitaji Roho Mtakatifu"?

353 Basi ni nani anayeweza kumtiisha ibilisi huyo? Mungu! Hatuwezi kufanya hivyo kwa dhehebu. Hatuwezi kufanya hivyo kwa nguvu za kikanisa. Lakini kulikuwako na Sauti wakati mmoja iliyofanya hivyo, amina, iliyowatiisha hao pepo, ikawapa akili timamu na kuwavalisha nguo. Sauti iyo hiyo ilitupa ahadi, "Kazi nizifanyazo mimi ninyi nanyi mtazifanya." Kamwe hutazifanya chini ya petroli ya kikanisa katika gari lililozibwa na kaboni. Hutaweza kufanya hivyo katika dhehebu. Utafanya hivyo hapo utakapojifanya tupu na kuwa dhaifu, ujimwage wote, na kumwacha Roho Mtakatifu aingie na kupapatisha kila sehemu yako, aloweshe kila kifuniko cha mwili wako. Hiyo ndiyo tu . . . kulifanya. Hatuhitaji dhehebu jipya.

354 Tunachohitaji, Ee Mungu, ninaisikia ikimwagikia hapa sasa. Tunachohitaji ni nabii wa Mungu kuinuka na radi ya Mungu, umeme wa kiroho utakaoutikisa ulimwengu huu uone aibu! Haleluya! Anachohitaji ni vyombo vitupu, hiyo ni kweli, Kanisa lililoitwa litoke, kundi la wachache litakalopokea nguvu za Mungu na baraka na Ujumbe Wake. Haleluya! Hicho ndicho tunachohitaji.

355 Kuwa dhaifu ili uweze kuwa na nguvu. Itashinda kila pepo. Itawaaibisha wenye elimu. Itawaleta wanaume na wanawake ambao Mungu amewaita, na hao pekee.

356 Kumbukeni, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu, watu wanane waliokolewa." Katika siku za Eliya kulikuwako na elfu saba tu waliokuwa Nayo. Loo, wazia tu mahali tunapoishi sasa. Wakati Yohana alipojitokeza jukwaani, maskini lile kanisa dogo bila shaka lilikuwa katika uchache, bali kulikuwako na vyombo vitupu vya kumiminia Mafuta. Haleluya!

Mungu, jalia tujifanye tupu.

357 Iweni tupu, enyi marafiki. Iweni dhaifu! Kanusha uwezo wako mwenyewe! Nanyi huko nje kwenye redio . . . sio redio, bali huko nje kwenye . . . mnaosikiliza kanda hizi, popote zinapokuja, jifanyeni tupu. Jimwageni juu ya madhabahu ya Mungu kama

dhabihu. Acheni Malaika aje na kaa la Moto, akijaze chombo hicho na nguvu za Mwenyezi Mungu. Pata...Ndipo atakutia nguvu, atakupa neema ya kusimama.

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja.

358 Ee Bwana, Jumapili nyingine asubuhi imepita, nasi tumekuwa tukiketi katika kusanyiko hili lenye uchaji, ambamo wanawake na wanaume wanaokujua Wewe, ambamo Roho Wako anaishi ndani ya mioyo yao, nao wanakuamini na wametimiza kila Neno ambalo Wewe—ambalo Wewe umetuagiza kufanya. Nasi tunakushukuru kwa ajili ya watu hawa.

359 Na huenda kukawa na wengine huko kwenye nchi ambako kanda hizi zitaenda, ambako maskini wanawake wanyenyekevu na wanaume watazipeleka nyumbani na kwenye makabila na huko nje kwenye nchi zingine. Basi jalia wasikie, Bwana, na wafahamu, wajifanye tupu kabisa kusudi Roho Mtakatifu aweze kuwajaza.

360 Huenda kukawa na wengine hata hapa asubuhi ya leo, Bwana, ambao wangeninii...wamejifanya tupu tangu tulipoanza kuzungumza, ambao wametambua ya kwamba wametegemea sana mawazo yao, kwa nafsi zao, wao...uwezo wao wenyewe, wakitegemea u—ujanja wa akili zao rahisi za kibinadamu, ambao si kitu ila uchafu mbele za Mungu. Ee Mungu, jalia wajifanye tupu tu sasa, kwa unyenyekevu wajitolee wenyewe na waje wakajazwe na Roho. Tujalie, Bwana.

Ilisema katika Biblia, "Wote walioamini walibatizwa."

361 Kwenye jengo hili asubuhi ya leo, Baba, ameketi maskini mwanamke mmoja, anayeketi hapa nyuma kule nyuma, nami ninamkumbuka Bibi Hicks akinijia usiku mmoja na hapo akalala akiwa tu si kitu ila mifupa mitupu, misuli, misuli midogo ya ngozi imekazikia mwilini mwake, kansa ilikuwa imemla; mumewe, hakuwa Mkristo bado. Nami ninakumbuka maombi niliyoomba usiku huo: "Mungu, Wewe ulimtuma maskini Daudi kumfuatilia simba akiwa na kombeo dogo rahisi, naye akamrejesha yule mwana-kondoo." Nikasema, "Kansa hii imemnasa dada yangu; yeye ni pepo. Ninajua Wewe ni Mungu. Nimekuona, Bwana, nami ninajua. Nimezungumza na Wewe, Nawe umenijibu." "Ninamfuatilia kondoo wa Mungu; kansa, mwachilie!" Ndipo nikamwagiza katika Jina la Yesu Kristo "Rudi nyumbani." Naye mumewe, ambaye hakuwa amejitoa bado, aliliamini Neno hilo na kumpeleka mkewe nyumbani. Huyu hapa asubuhi ya leo, mwanamke mkubwa mwenye afya, kansa imetoweka, yuaja asubuhi ya leo kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Ee Mungu, asante kwa ajili ya hicho chombo kitupu kilicho tayari kujazwa. Mungu, ninaomba ya kwamba utaibariki nafsi hiyo.

362 Bwana, huyo ni mfano tu wa wengine wengi. Ninaomba ya kwamba baraka Zako zikae juu ya kusanyiko hili, kwa uchaji, Mungu, kwa uchaji. Iwapo . . .

363 Lipo jambo moja tu lililosalia, Baba, ninaloweza kuona, hilo ni, ama usimame mahali fulani ukiwa na vyombo vitupu na kuufanya ulimwengu huu ujionee aibu, ama umtume Yesu mara moja. Kwa kuwa mwisho umewadia, Bwana, kuna mambo mawili tu yaliyosalia kufanywa (nasi hatuna budi kuyaona mara moja) kwa kuwa tunajua ni mwisho; ama tutaona kitu fulani kikuu kikiinuka mara moja, au tutakuona kule Kuja kwa Bwana.

364 Unabii wote umetimizwa. Jambo la mwisho kabla Kanisa halijafufuliwa, kabla halijatwaliwa katika Ufunuo mlango wa 3, lilikuwa ni kule kuja kwa mjumbe kwa Wakati wa Kanisa la Laodikia, ambaye "angeigeuza mioyo ya watu iwarudie akina baba wa mwanzoni," kuwarudisha kwenye Pentekoste ya kawaida, kile wanachodai kuwa nacho. Kungekuwako na maelfu mara maelfu, kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, Bwana, wangepotea. Wengi wao wangepotea. Tunaona hilo tayari limetimizwa, Baba.

365 Njoo, Bwana Yesu, linyakue Kanisa Lako. Na kama ni mapenzi Yako, Bwana, kabla tu Kanisa hilo halijanyakuliwa, jalia Nguvu ziinuke. Ee Mungu, vijaze vyombo hivi. Wainue, Bwana! Utikise ulimwengu huu mara nyingine tena! Tunajua wakati utakuwa umekwisha, hakutakuwako na toba wakati huo, watakuwa wamechelewa sana wakati huo. Bali onyesha Nguvu Zako, Bwana, vijaze vyombo hivyo na uutikise ulimwengu huu jinsi ambavyo haujapata kutikiswa hapo awali! Lichukue Kanisa Lako basi. Uache ulimwengu katika mchafuko uliomo, Ee Mungu, wanapambana.

366 Ndipo tunajua Roho Mtakatifu mkuu atawajilia Wayahudi basi. Tulipowaona wale mia moja arobaini na nne elfu wamesimama juu ya Mlima Sinai, wamesimama pamoja na Mwana-Kondoo, bali Bibi-arusi alikuwa Mbinguni tayari. Alikuwa tayari ametwaliwa juu, naye Mwana-Kondoo alikuwa amerudi (Yusufu) akajitambulishe kwa watu Wake. Nayo Biblia inasema ya kwamba kutakuwa na huzuni miongoni mwao hapo watakapoangalia na kumwona Yeye amesimama pale. Wakati atakapojitambulisha, wao watasema "Ulipata wapi makovu hayo?"

Akasema, "Katika nyumba ya rafiki Zangu."

Ndipo watasema, "Kumbe ni Yule tuliyemsulibisha."

367 Naye atasema kama Yusufu alivyosema, "Msiwe na wasiwasi, kwa kuwa Mungu alifanya jambo hili apate kuyaokoa maisha ya Mataifa. Hayakuwa ni makosa yenu." Ndipo walisema watatengana, familia moja na nyingine, wangeomboleza kama kwamba mwana wa pekee ameondolewa nyumbani.

368 Ee Baba, siku hiyo imekaribia, huko ni kumalizika kwa yale Majuma Sabini. Wakati huo umewadia, Bwana.

369 Ee Mungu, jalia sauti—sauti ya manabii wa kweli wa Mungu ilie dhidi ya mama huyu wa kisasa wa siku hizi, kanisa hili la kisasa, theolojia hii ya kanisa la kisasa.

370 Watikise wahubiri hawa wanaoogopa kusema Ukweli. Ee Mungu, wachukue watu hawa na kuwatikisa kama vile hawajatikiswa awali, wafanye wajionee aibu.

371 Lakini tunajua jambo hili moja, nasi tunaweza kutulia kwa matumaini makamilifu, ya kwamba, "Hakuna mtu atakayekuja asipovutwa na Baba. Na wote alionipa Baba watakuja." Watafikia umbali ule tu unaotarajia wafike. Ila Wewe ulisema, "Msiogope, enyi kundi dogo, Baba yenu ameona vema kuwapa ninyi Ufalme." Tunajua Hiyo ni kweli. Ulituonya kote kote kwamba ni wachache sana watakaokuwa tayari wakati huo utakapotimia. Ndipo kutakuwako na ufufuo mkuu, na wote waliokombolewa ambao wamekombolewa kote katika nyakati wangefufuka. Lakini katika siku hii ya mwisho, kwenye wakati tu wa mwisho, hapo Kanisa hakika lingekuwa katika uchache.

372 Kwa hiyo tunauona huo, Baba, tunauona Ujumbe wa siku hii. Tunaona kukataliwa Kwake, tunaona mitengano, tunaona mambo haya yote.

373 Tunawaona watu Wako wakikiri ya kwamba wao si ninii . . . wao "si kitu." Wanataka tu kujazwa na Wewe, Bwana. Sasa, ninaomba ya kwamba utautikisa ulimwengu pamoja nao, siku chache tu kabla ya Kuja kwa Bwana.

374 Sasa miongoni mwetu mna ugonjwa, wapo watu wanaohitaji uponyaji wa kimwili. Tusingeweza kuwaacha, Bwana, kwa kuwa imesemwa, "Usisahau fadhili Zake zote: Yeye akusameheaye uovu wako wote; Naye huyaponya magonjwa yetu yote." Tunaomba ya kwamba nguvu Zake kuu za uponyaji zitakuwa juu ya kila mmoja aliye hapa. Kama unaweza kuokoa nafsi huko nje pasipo kusogea, moyo wake tu ukiwa umeelekezwa Kwako, ni zaidi sana kiasi gani unavyoweza kuuponya mwili!

375 Hizi hapa leso zimewekwa hapa. Ninazibariki katika Jina la Bwana Yesu, kama vile yule Mtume mkuu Paulo alivyofanya. Jalia yeyote atakayezivaa leso hizi aponywe. Jalia familia zilizovunjika ziimarishwe tena. Jalia watoto wadogo, wasio na baba, wasio na mama, nao wametengana, jalia familia hiyo iunganishwe tena. Tujalie, Bwana. Waponye wagonjwa wote sasa, na wanaoteseka, jitwalie utukufu kwako Mwenyewe.

376 Na, Bwana, sisi tunaojaribu kuviweka vyombo vyetu juu, macho yetu juu, mioyo yetu juu kukuelekea Wewe, tukikanusha kwamba hata tumehusishwa katika ulimwengu huu. Biblia ilisema ya kwamba "Ibrahimu alitoka nyumbani mwake, akatoka kwenye mji wake, kusafiri katika nchi ya ahadi, akikiri ya kwamba yeye 'hakuwa ni wa ulimwengu huu' bali alikuwa ni

'msafiri na mgeni.'" Ibrahimu na Isaka na Yakobo, wote walio na ushuhuda huu ya kwamba wao "si wa ulimwengu huu," wao kwa urahisi wanatangaza ya kwamba kuna Mji ambao Mwenye Kuubuni na Kuujenga ni Mungu, nao wanaelekea huko.

377 Jalia mioyo ibadilishwe sasa hivi wakati ninapoomba, Baba, na jalia misimamo ichukuliwe. Na wakati ibada za ubatizo zitakapokuja, jalia kuwe na uamsho mkubwa sana miongoni mwa watu, jalia pawepo na watu ambao hawakuwa wameuwazia hapo kabla, jalia ufunuliwe. Nawe ulisema wote uliokuwa umewaita, Wewe—Wewe utawapeleka.

378 Sasa, ninawakabidhi wote Kwako, Bwana, pamoja na maskini ujumbe huu uliovunjika-vunjika kutoka kwenye chombo duni kilicho tupu, Bwana. Ninaomba ya kwamba utayachukua tu Maneno hayo Nawe utayayeyushia mioyoni mwa watu, na hebu kamwe wasiweze kuliondokea. Tujalie, Bwana. Ninayakabidhi Kwako sasa, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

379 [Ndugu mmoja anatoa ujumbe—Mh.] Wakati mkiamua, jiamulieni. "Kwa nini mnasita-sita katika mawazo mawili?" Mlisikia alivyosema. Mungu akiwa Ndiye Mungu, mtumikieni; ulimwengu ukiwa ndio mungu, endeleeni tu. Mnaona? Njia ya kimadhehebu ikiwa ndiyo kweli, endeleeni nayo; bali kama Biblia ndiyo kweli, basi njoni Kwake. Mnaona? Chagueni saa hii yule mtakayemtumikia.

380 Hebu tuninii, katika Roho, tuimbe wimbo sasa. Biblia ilisema, "Waliimba wimbo kisha wakatoka." Hebu na tuimbe wimbo huu wa kale unaojulikana sana, *Nampenda*, huku kichwa chetu na mioyo imeinamishwa Kwake.

Nampenda,

Sasa amua yale utakayofanya.

Nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

381 [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Nampenda*—Mh.] Je! waweza kufanya uamuzi wako kwa ajili ya Kristo? Sio uamuzi, hasa, jifanye tupu tu, "Bwana, mimi si mwema. Hakuna kitu ndani yangu kilicho kizuri. Jalia nisahau yote niliyopata kujua. Sasa njoo, Bwana Yesu, usiliache hili lipitie juu ya kichwa changu. Jalia nilipokee na kujazwa na Roho Wako, Bwana. Tangu siku ya leo na kuendela, jalia niwe Wako kabisa." Ombeni tu sasa, maombi mafupi tu kwa Mungu; rahisi, maombi haya, enyi watoto, wote.

Ewe Mwana-Kondoo wa Kalvari,
Mwokozi wa kiungu; (tubu tu moyoni mwako)
. . . nisikie niombapo,
Ondoa dhambi zangu zote,
Jalia tangu leo hii
Niwe Wako kabisa!

Ninapotembea kwenye matatizo ya maisha
yenye giza,
Na hofu zinaenea kunizunguka,
Kuwa Kiongozi Wangu;
Agiza giza ligeuke kuwa mchana,
Pangusa huzuni, hofu,
Wala usiniache nikaondoka
Karibu na Wewe.

382 [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Imani Yangu Inakutegemea*—Mh.] Hawa ambao wameamini, uliyejifanya tupu mbele za Mungu, na umekusudia ya kwamba hakuna kitu kitakachokuzuia tena, kamwe hutakiri uwezo wowote, na unataka kuufanya dhahiri, mzuri na halisi kwa Mungu, kidimbwi kina maji ndani yake, kikiandaliwa kwa ajili ya ubatizo. Hebu wanawake waende mkono wangu wa kuume, na wanaume mkono wangu wa kushoto. Ibada ya ubatizo itakuwa hivi punde tu. Wale ambao wamejifanya tupu, mko tayari kutoamini yale wahudumu wasemayo, yale mapadre wasemayo, kile madhehebu yasemayo, bali mtachukua njia ya Bwana, mtaamini BWANA ASEMA HIVI, njoni sasa.

Ninapotembea kwenye matatizo ya maisha,

Hao watakuwa ni wanawake *huku*, wanaume *huku*. Huo ndio wito wako wa madhabahuni, "Wote walioamini, walikuja wakabatizwa."

. . . Kiongozi Wangu;
Agiza giza ligeuke mchana,
Pangusa machozi ya huzuni,
Wala usiniache nikaondoka
Karibu na Wewe.

383 Ni wanawake wangapi humu ndani asubuhi ya leo. . . Ninasema hili katika Jina la Bwana Yesu! Ni wangapi wenu mnaoona aibu kwa ajili ya nywele hizo fupi mlizo nazo, mnamtaka Mungu (kwa neema Yake) kuiacha ikue kwa ajili yenu? Mungu awabariki.

384 Ni wanaume wangapi wanaona aibu kwamba umemwacha mke wako avute sigara, na kuvaa suruali ambayo kwa kweli ni zako?

385 Nayo Biblia ilisema, "Ni chukizo machoni pa Mungu." Hivi mnajua Mungu hawezi kubadilika? Yeye hawezi kubadilika. Yeye ana tabia moja, hiyo ni utakatifu. Hawezi kubadilika. Kama hutafanana Naye, wewe hutamwona, "Pasipo utakatifu

hapana mtu atakayemwona Bwana." Na kama kuvaa suruali fupi ni . . . inamfanya Mungu kuchefuka tumboni Mwake na kutapika, anachefuka, na *chukizo*, "uchafu," kamwe utawezaje . . . una roho kama huyo ndani yako na kweli utafika Mbinguni? Utafikaje Mbinguni ukiwa na nywele fupi, wakati Mungu alisema "Ni aibu kwa mwanamke kukata nywele zake"? Yeye anakana kanuni zenyewe za kuwa m—mke. Mungu habadiliki. Hilo ni Neno Lake, ewe rafiki, afadhali usikilize.

386 Nanyi wanaume mtakaowaacha wake zenu wafanye hivyo, hivi hamjionei aibu? Hamwoni aibu?

387 Msiwe kama Mama Taifa wa nchi. Iweni kama Mungu! Mnaona? Jifanyeni tupu kutokana na mwelekeo huu wa kisasa wa ulimwengu, kusudi Kristo aweze kujimimina Mwenyewe ndani yenu nanyi mweze kujazwa kweli na Roho Mtakatifu.

388 Hawezi kufanya hivyo, hawezi kufanya hivyo, ni—ni kinyume cha kanuni Zake; ingembidi kulikiuka Neno Lake, na hilo Yeye hatalifanya; hatafanya hivyo mradi—mradi huambatani na Neno Lake. Inakubidi kuja . . . Inatubidi kulijia Hili kabla jambo lingine lolote kufanywa. Mnajua hilo, kila mmoja wenu anajua hilo. Ni wangapi wanaoamini hilo, inua mkono wako. Hakika, mnaliamini, sasa hebu na tufanye jambo kulihusu.

389 Mungu, uturehemu! Jinsi tunavyomhitaji! Sisi hapa, sote pamoja sasa. Kumbukeni sasa, kwenye ile Hukumu, kama mimi . . . Itanibidi kusimama (na hiyo huenda ikawa ni kabla ya usiku wa leo) na kukabiliana na kila Neno ambalo nimesema. Mnaona, itanibidi kukabiliana nalo. Sasa, kumbukeni ya kwamba uovu umeondoka mikononi mwangu, umeondoka kwenye dhamira yangu, umeondoka kwenye nafsi yangu, umeondoka kwa Mungu.

390 Kama hutaninii . . . Kama unasimama katika hali hizo na ungali hujisikii kuhukumiwa (whiu!), u—u—utafanya nini? Basi unajua Mungu hakushughulikii, unajua umepita Hapo. Unaona? Umepita Hapo. Huenda ukawa ni wa kidini sana, huenda ukawa mfuasi wa makanisa na kadhalika, bali umepita Hapo. Neno la Mungu hushuka likaingia ndani na kumtoa mtu nje. Hicho ndicho kitu kinachowarudisha. Mnaona? Kwa hiyo hilo ni Neno. Ninamuuliza mhudumu yeyote, mtu yeyote, mahali popote, kukanusha Hilo dhidi ya Neno la Mungu. Hiyo ni kweli. Si hivyo, mnaona.

391 Kwa hiyo hebu na tuwe Wakristo halisi. Hata sisi tunaojaribu, wale wanaojaribu, tunahitaji kukatwa na kuchemshwa tena. Naam, bwana, sote tunahitaji hilo.

392 Mungu, unirehemu. Mungu, nitwae na unifinyange. Ni kusudi langu, baada ya juma hili, kwenda mbele za Mungu, nipate kujua ni nini kingine cha kufanya. Mungu, nitwae. Ninii . . . Yo—yote yananihusu mimi (na kuna mengi) yasiyo mazuri, Mungu, yakatilie mbali, ndiyo maombi yangu asubuhi

ya leo. Tahiri moyo wangu, masikio, utu wangu. Nifanye, Bwana, nifanye kitu ambacho . . . chochote anachotaka niwe. Hayo ndiyo maombi yangu.

393 Chochote ninachohitaji kuwa, kikatilie mbali, nikatilie mbali, Bwana. Nionyeshe kwenye Neno, niambie, nitaenda nilifanye. Hebu Bwana aliseme, nami nitaninii . . . Niko pale pale nikiwa tayari kulitekeleza. Chochote Neno la Bwana lisemacho, hicho ndicho ninachotaka kuwa. Ninataka kuwa M—Mkristo katika Neno la Mungu, "Nikiliacha neno la kila mtu liwe ni uongo, na la Mungu liwe kweli." Huo si ungekuwa ndio mwelekeo wa wakati, si ungekuwa ni huo? Hivyo ndivyo mnavyoliamini?

394 Je! unatafuta mahali pa kubatiziwa, mwanangu? Naam, hapa nyuma, ndugu, usingojee. Vema, moja kwa moja upande huu.

395 Wengi wenu mnapaswa kuwa mkija, wanaume na wanawake ambao ni waaminio, ambao wananinii . . . wanakiri dhambi zao, kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo. (Upande huu, ndugu.) "Katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zao, nao watajazwa na Roho Mtakatifu."

396 Sasa, kwenu Wakatoliki hapa, hilo ndilo ondoleo la dhambi. Mnasema kanisa lina mamlaka ya kuondoa dhambi, kanisa liliondoaje dhambi? Mungu . . . Yesu aliliambia kanisa, "Wowote mtakaowaondolea dhambi, wameondolewa. Na wowote mtakaowafungia dhambi, wamefungiwa." Waliziondoaje za kwanza, dhambi katika kanisa la mwanzoni? Waliwaagiza watubu, nao wakawabatiza katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zao. Sio chini ya kibanda cha kutubia; la, hasha. Bali walitubu mbele za Mungu, mioyoni mwao wakati walipokuwa wamesimama pale, nao wakaamini. "Na wote walioba- . . . walioamini walibatizwa katika Jina la Yesu Kristo, nao wakajazwa na Roho Mtakatifu." Amina. Mnampenda?

Sasa hebu na tusimame.

397 Sasa, kutakuwako wengi watakaopenda kuingojea ibada ya ubatizo. Yeyote mwingine anayetaka kuja, yeyote mwingine ambaye ameamini? Njoo, upande mmoja wao; wanaume mkono wa kushoto; wa kulia, wanawake. Mwamini Bwana Yesu kwa moyo wako wote, kwa yote yaliyo ndani yako.

398 Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu pamoja, wakati tukirudia ombi hili rasmi pamoja, kwani ninajisikia kuongozwa kiajabu sana kufanya jambo hili sasa hivi. Tunapoinamisha vichwa vyetu, ninyi ombeni pamoja nami. [Ndugu Branham na kusanyiko wanaomba kwa pamoja—Mh.]

. . . *Baba yetu* Uliye *mbinguni, Jina lako litukuzwe,*

*Ufalme wako uje, Mapenzi* yako *yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni.*

*Utupe leo riziki yetu.*

*Utusamehe* makosa *yetu, kama sisi nasi tunavyowasamehe* wanaotukosea.

*Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu: Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina.*

399 Sasa hebu na tuendelee kuinamisha vichwa vyetu. Nami nitamwomba Ndugu Neville aje atuombee baraka, aseme kile kilicho moyoni mwake, kisha atangaze kuhusu ibada ya ubatizo ambayo inaandaliwa sasa.

400 Mungu awabariki, ndilo ombi langu. Nitawaombea, ninyi niombeeni. Kweli ninahitaji maombi yenu.

*Uweza Mkamilifu Kwa Udhaifu Mkamilifu* SWA61-1119
(Perfect Strength By Perfect Weakness)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham ulihubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 19 Novemba, 1961, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani. Kila jitihada imefanywa kuuhamisha kwa usahihi Ujumbe huu wa sauti kutoka kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa hadi kwenye ukurasa uliochapishwa, na umechapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani  kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org